

**MIELEKEO YA WALIMU WA SHULE ZA MSINGI KUHUSU SUALA LA
LUGHA KAMA LINA VYOELEZWA KATIKA KATIBA YA KENYA**

ROSE KAUMEURU MIRIANGA

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA
SHAHADA YA UZAMILI KATIKA TAALUMA YA KISWAHILI, CHUO KIKUU CHA
NAIROBI**

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na wala haijawahi kutolewa katika chuo kingine chochote ili kutahiniwa kwa mahitaji ya Shahada.

Sahihi..... Tarehe.....

ROSE KAUMEURU MIRIANGA

Mtahiniwa (C50/79831/2012)

Tasnifu hii imewasilishwa ili kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu Cha Nairobi kupitia Idara ya Kiswahili.

Sahihi Tarehe

DKT. AYUB MUKHWANA

(Msimamizi)

Sahihi Tarehe

DKT. IRIBE MWANGI

(Msimamizi)

TABARUKU

Kazi hii naitabarukia Mamangu mpendwa Elizabeth Kabutia Mirianga, Marehemu babangu Peter Mirianga, Kakangu mpendwa Japhet Mukaria na Mume wangu mpendwa Shadrack Mithika.

SHUKRANI

Ninatoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwa kunipa siha njema hadi nikaweza kuikamilisha kazi hii.

Juhudi za kuikamilisha tasnifu hii hazikukosa changamoto kadhaa. Hata hivyo imekamilika kutokana na mchango wa watu mbalimbali. Ukarimu, juhudi na hisani za watu hawa zilituwezesha kufaulisha kazi hii.

Shukrani tele kwa wasimamizi wangu Dkt. Ayub Mukhwana na Dkt. Iribe Mwangi kwa kunielekeza tangu mwanzo hadi tamati ya tasnifu hii. Ustahimilivu, uelekezi na uongozi wao wa kitaaluma ulinifaa katika ulimwengu wa usomi kwa njia ya kipekee. Mungu awaongeze hekima.

Nawashukuru wahadhiri wengine walionishauri na kuniandaa kiusomi hadi nikaweza kuikabili kazi hii. Shukrani zangu ni kwa; Prof. John Habwe, Prof. Abdullaziz Mohamed, Prof. Kithaka wa Mberia, Prof. Wamitila Kyalo, Prof. Mwenda Mbatiah, Prof. Kineene wa Mutiso, Dkt. Alfred Buregeya, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Swaleh Amiri, Dkt. Tom Olali na Bw. B. G. Mungania.

Ninawashukuru wanafunzi wenzangu tulioabiri pamoja katika safari hii. Ahsanteni kwa kunihimiza hadi nikafikia hapa. Mungu awabariki Ann Njoroge, Mary King'ora, James Mburu, Ann Raitania, Karoki Emaita, Kilanga Simon na Millicent Sabula.

Shukrani za dhati zikufikie Ndugu Hezekiah Gikambi kwa kunipa motisha na kujitolea si haba nilipohitaji msaada wako. Mungu akuongeze hekima tele.

Shukrani za dhati kwa mume wangu Shadrack Mithika kwa kunitia moyo na kunivumilia katika

kipindi hiki cha masomo. Asante kwa ufadhili wako katika masomo yangu. Aidha, asante watoto wetu wpendwa; Lorna Mwende, Amy Kendi, Hope Gatwiri na Angel Gakii. Niliwanyima muda wenu ili niweze kutimiza ndoto yangu. Mungu awawezeshe kusoma na kutimiza ndoto zenu.

Ningependa pia kuwashukuru marehemu babangu Bw. Mirianga, mamangu Bi. Mirianga, ndugu zangu na watoto wao. Bankwe na mamkwe Bw. na Bi. Thiuri, wifii na shemeji zangu wote, nawashukuru kwa kunihimiza na kunishauri hadi kiwango hiki cha uzamili. Mola awajalie baraka tele.

Rafiki zangu ambao haitawezekana kuwataja wote kwa majina, asanteni kwa kunishauri na kunitia moyo katika masomo yangu.

IKISIRI

Nchini Kenya, walimu wa shule za msingi ni kielelezo cha kuigwa na wanajamii walio wengi hasa katika maeneo ya mashambani. Aghalabu, wanayoyatenda na wanayoyasema walimu hawa kuhusiana na lugha ndiyo yanayofuatwa na wanajamii walio wengi. Tasnifu hii ni uchunguzi wa mielekeo ya wadau hawa muhimu kuhusu majukumu yaliyotengewa lugha mbalimbali, ukuzaji na uendelezaji wa matumizi ya lugha kama inavyoangaziwa na kauli za Katiba ya Kenya zihusuzo suala la lugha. Mielekeo ya wadau hawa inatarajiwa kuwa mwongozo kwa waundaji sera ya lugha na pia wapangaji lugha ili kubuni mikakati ya kuhimiza ushawishi na uhusika wa walimu husika, kama wadau muhimu, katika kutekeleza sera ya lugha kama inavyojitokeza katika Katiba ya Kenya ya mwaka wa 2010. Uchunguzi huu ulijikita nyanjani ambapo data ilikusanywa kwa njia ya hojaji, mahojiano na utazamaji wa tabia za watafitiwa kuhusu lugha ya Kiswahili, Kiingereza na lugha asilia (Kimeru). Kutokana na matokeo ya utafiti huu, mielekeo ya watafitiwa kuhusu suala la lugha kama linavyojitokeza katika Katiba ya Kenya, imetokana na masiala ya kihistoria, kijamii, kiisimu na kiuchumi. Uchanganuzi wa data ya utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Kijamiinafsia iliyoasisiwa na Lambert (1963) na ile ya Kijamii ya Fishman (1972).

SURA YA KWANZA

1.0 Usuli wa Mada

Hadhi ya lugha fulani na thamani yake katika jamii hutegemea kwa kiasi kikubwa mielekeo ya wadau mbalimbali wa kimsingi katika mchakato wa utekelezaji wa sera ya lugha kuhusu majukumu yaliyotengewa lugha hiyo katika jamiilugha husika. Utafiti huu unajikita katika mielekeo ya walimu wa shule za msingi wa wilaya ya Igembe Kaskazini kuhusu suala la lugha kama linavyoelezwa katika Katiba ya Kenya iliyopitishwa mwaka wa 2010.

Ingawa dhana ya mielekeo imefasiriwa kwa namna tofautitofauti na wataalamu mbalimbali, baadhi ya wataalamu hao wametuelekeza katika kufahamu dhana hii kama hali ya kiakili ya mtu inayotokana na kichocheo cha aina fulani na hali hii inaweza kuathiri namna mtu huyo anavyoitikia kwa njia kubalifu au isiyo kubalifu kuhusu kitu au jambo fulani (taz. Allport, 1954:24, Ngidi, 2007:9). Mielekeo kuhusu lugha huwa hisia chanya au hasi wanazodhihirisha watu wanapojipata katika hali zinazowahitaji kufanya teuzi miongoni mwa lugha na hali tofautitofauti za matumizi ya lugha (Smith 1996:147).

Hisia za watu kuhusu lugha zaweza kuhusu lugha yao, lugha za wengine na vilevile lugha zote kwa jumla. Lugha ya wanajamii walio wengi mara nyingi huchukuliwa kama lugha iliyo bora. Watu huamini kwamba lugha ya walio wengi (kama vile lugha ya taifa) ina hadhi ya juu kijamii na kwa kuitumia, wazungumzaji hupata hadhi ya juu ya kiuchumi kwa sababu inawawezesha kupata fursa bora zaidi za kikazi na kujiinua kimaisha au watoto wao siku za usoni. Wanaweza pia kufikiria kuwa lugha yenye jukumu la kitaifa ndiyo bora zaidi kwa sababu inawawezesha kudhihirisha uzalendo wao na kuongeza mshikamano wao katika taifa husika. Watu wengine wanaweza kufikiria kuwa lugha isiyo na othografia sio lugha kamili. Wanajamiilugha kama

hawa wanaweza kuona aibu wanapoitumia lugha kama hii yao hadharani (taz. Mohochi, 2011:24)

Mielekeo ya wanajamii kuhusu lugha huwa sehemu ya utamaduni wao wa matumizi ya lugha, ambapo sera ya lugha katika jamii husika huwa na msingi katika utamaduni huu (Schiffman 1996). Walimu wa shule za msingi ndio wadau wa kimsingi katika mchakato wa utekelezaji wa sera ya lugha. Walimu hawa wana ushawishi mkubwa sana kutokana na nafasi wanayoshikila katika jamii. Wadau hawa wameenziwa na kuheshimiwa kwa sababu ya maarifa waliyo nayo kuhusu matumizi ya lugha tofautitofauti. Mara nyingi wanajamii wengine hupenda kuiga wayafanyayo walimu, hali inayobainika pia katika matumizi ya lugha. Kwa sababu hii mienendo na maoni yao kuhusu lugha husika yanadhihirisha mielekeo yao kuhusu majukumu yaliyopewa lugha katika jamii husika. Mielekeo ya washikadau kama vile walimu wa shule za msingi huenda ikawa wazi au isiwe wazi, lakini huathiri utekelezaji wa sera ya lugha nchini Kenya kwa njia chanya au hasi.

Jumla ya kanuni zilizokubaliwa na wananchi, ambazo hutumiwa kuendesha shughuli za nchi hujulikana kama katiba ya nchi husika (TATAKI, 2013:201). Katiba ni jumla ya kanuni za kimsingi zinazotumika katika kuitawala nchi, hasa zinapojumuishwa katika haki za raia wa nchi husika (McKeown 2008:358). Kauli za Katiba ya Kenya kuhusu lugha zinaakisi sera ya lugha inayotambua na inayosisitiza wingilugha katika kiwango cha kitaifa. Kwa mujibu wa kauli za katiba ya Kenya zinazohusu suala la lugha, serikali inataamali kutekeleza sera ambapo lugha zote zinazozungumzwa nchini Kenya zitakuzwa. Vilevile, mahitaji ya kilugha ya watu wenye changamoto za kimaumbile kama vile Lugha Ishara ya Kenya na Breli, yameshughulikiwa katika Katiba ya Kenya (Katiba ya Jamhuri ya Kenya, 2010:22).

Kwa mujibu wa Sura ya 2, Ibara ya 7, sehemu ya (1) hadi sehemu ya (3), lugha ya Kiswahili kama mojawapo ya lugha za kienyeji imepewa jukumu la lugha ya taifa la Kenya. Vilevile lugha ya Kiswahili imekwezwa kihadhi na kuwa lugha rasmi Kenya, sambamba na lugha ya Kiingereza. Aidha, serikali imenuia kukuza na kuendeleza matumizi ya lugha tofautitofauti za wakenya. Matumizi ya lugha za kiasili, Lugha ishara ya Kenya, Breli na njia nyingine za mawasiliano na teknolojia zinazoweza kufikiwa na watu wenye ulemavu yamenuiwa kulindwa na kustawishwa na serikali ya Kenya.

Kuteuliwa kwa lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa na kuongezewa jukumu la kuwa lugha rasmi sambamba na Kiingereza kutasaidia lugha hii kutumika katika nyanja tofautitofauti nchini Kenya. Jambo hili pia litasaidia katika ukuaji na ustawi wa lugha hii. Ingawa utambuzi wa lugha za Wakenya unadhihirika katika Katiba ya Kenya, swali linaloibuka ni je, ni masharti yapi yanayoongoza matumizi ya lugha hizi nchini Kenya? Inatubidi tujiulize pia ni nini hatima ya lugha nyingine asilia zinazodhihirisha utambulisho wa wanajamiilugha husika ikilinganishwa na Kiswahili, lugha asilia iliyokwezwa kihadhi na kupata majukumu muhimu sana katika jamii.

Maoni ya wataalamu kama vile King'ei (2010) na Mukhwana (2008) ni kwamba sera ya lugha nchini Kenya imekuwa na utata tangu nyakati za ukoloni (1895-1963). Mielekeo ya wataalamu hawa ni kwamba kukwezwa kwa Kiingereza juu ya lugha zote nchini Kenya ni hali inayoendelea kutinga maendeleo ya Kiswahili na lugha nyingine asilia hasa kupitia sera ya lugha katika sekta ya elimu. Wanajamii basi wamekuwa wakikionea fahari Kiingereza kama lugha inayoweza kuwaletea ufanisi wa kikazi katika jamii. Hii ni kwa sababu kutoka nyakati za ukoloni, lugha ya Kiingereza imenasibishwa na elimu bora ambapo elimu bora kwa wengi ni daraja ya kupata ajira nzuri (Mukhwana, 2008:2).

Baadhi ya watafiti kama vile Mohochi (2011), wamelalamikia hali ambapo hata wasomi Waafrika na ambao ni wataalamu wa Kiswahili hupendelea kutumia lugha ya Kiingereza katika mawasilisho ya makala katika makongamano, mikutano ya kitaaluma na pia katika kuchapisha majarida mbalimbali ya kiakademia yanayojadili kuhusu lugha ya Kiswahili. Mohochi anaeleza kuwa miongoni mwa majarida 33 yenye mada za Kiswahili, majarida yaliyoandikwa kwa Kiswahili ni 7 peke yake, kwa mfano katika jarida la *Nordic Journal of African Studies*. Mohochi anawalaumu wataalamu kama hawa wa Kiafrika ambao wanadhihirisha mielekeo hasi inayoonyesha dhara kwa lugha ya Kiswahili. Kwa mujibu wa mtaalamu huyu, ni mielekeo kama hii ambayo inachangia hali ya kudunisha lugha hii na kukwaza uendelezaji wake (uk.34-35).

Kama tulivyodokeza hapo awali, Wakenya wengi hasa waliosoma hupendelea na kuonea fahari matumizi ya lugha ya Kiingereza hasa katika miktadha rasmi, huku lugha ya Kiswahili na lugha nyingine asilia zikidharauliwa. Ili kustawisha na kuendeleza matumizi ya lugha zote na tamaduni zinazoandamana na lugha hizi, ni muhimu kuzipa nafasi nzuri katika mfumo wa elimu hasa ile ya msingi. Ni muhimu pia kuondoa kasumba kuwa lugha asilia zinaashiria ukabila au utamaduni uliopitwa na wakati, kasumba iliyoenezwa na sera ya lugha ya wakoloni nchini Kenya na kuangamiza matumizi ya lugha za Kiafrika.

Utafiti huu una matarajio kwamba sera ya lugha nchini Kenya, kama inavyoelezwa katika Katiba ya Kenya bado inaweza kuzua mielekeo tofautitofauti kutoka kwa washikadau wa kimsingi ambao ni walimu wa shule za msingi. Uchunguzi unaoangazia mielekeo ya washikadau hawa ni muhimu katika kubaini ufahamu na ukubalifu kuhusu majukumu yaliyopewa lugha mbalimbali, uhusika wao pamoja na ushawishi wao katika mchakato wa utekelezaji wa sera ya lugha nchini

Kenya kama inavyojitokeza katika Katiba ya Kenya. Hili huwawezesha waunda sera ya lugha na vilevile wapangaji lugha kubuni mikakati zaidi inayohitajika ili kufaulisha mchakato huu.

1.1 Tatizo La Utafiti

Utafiti huu ulinuia kuchunguza mielekeo ya walimu wa shule za msingi kuhusu suala la lugha kama linavyojitokeza katika Katiba ya Kenya. Katika jamii yenye wingilugha kama ilivyo Kenya, mielekeo ya wanajamii kuhusu majukumu yanayohusishwa na lugha mbalimbali huwa tofautitofauti. Utafiti huu hivyo basi ulichunguza mielekeo ya walimu wa shule za msingi kama washikadau muhimu wa mashinani katika mchakato wa utekelezaji wa sera ya lugha nchini Kenya. Mielekeo na ukubalifu wao kuhusu sera ya lugha kama inavyoelezwa katika Katiba ya Kenya ilitarajiwa kuwa na ukinzani. Kwa sababu hiyo, utafiti huu ulilenga kutaka kubaini mielekeo ya walimu hawa kuhusu suala la lugha kwa kuzingatia kauli zinazohusu suala hili la lugha katika Katiba ya Kenya ya mwaka wa 2010.

Kwa kuchunguza mielekeo ya walimu wa shule za msingi tunaweza kutathmini uhusika na ukubalifu wao na hivyo, ushawishi wao katika utekelezaji wa sera ya lugha nchini. Maana ya sera ya lugha katika kazi hii imeongozwa na ufafanuzi kuwa ni maamuzi yanayofanywa na watawala pamoja na wanasheria kuhusu uteuzi wa lugha mbalimbali ili kutekeleza majukumu mbalimbali nchini Kenya (Mukhwana 2008:16). Maamuzi haya nchini Kenya yanadhihirika katika kauli za Katiba ya Kenya zinazozungumzia suala la lugha ambalo linahusu majukumu, ukuzaji na uendelezaji wa matumizi ya lugha mbalimbali za Wakenya. Utafiti wetu uliongozwa na mtazamo kwamba mielekeo ya washikadau wa kimsingi kuhusu matumizi ya lugha ni muhimu katika mchakato wowote unaohusisha sera ya lugha. Mtazamo huu unaungwa mkono na Jones (2012), anayeeleza kwamba mielekeo ya washikadau kama vile walimu hubainisha ukubalifu na uhusika wao katika utekelezaji wa sera ya lugha nchini Kenya. Kwa sasa hakuna

ithibati kuwa wadau tuliowatafiti walihusishwa katika suala la lugha katika Katiba ya Kenya 2010. Wadau hawa wa lugha wanalihusishwa katika suala hili la lugha, hakungalikuwa na Katiba mpya Kenya na hali ya lugha isingalibakia ile ile ya awali.

1.2 Madhumuni ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza mielekeo ya walimu wa shule za msingi kuhusu suala la lugha kama linavyoelezwa katika Katiba ya Kenya ya mwaka wa 2010.

Utafiti wetu uliongozwa na madhumuni mahsusi yafuatayo:

- i. Kuchunguza mielekeo ya walimu wa shule za msingi Wilayani Igembe Kaskazini kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha ya taifa na lugha rasmi nchini Kenya.
- ii. Kuchunguza mielekeo ya walimu wa shule za msingi Wilayani Igembe Kaskazini kuhusu matumizi ya Kiswahili na Kiingereza kama lugha mbili rasmi shuleni.
- iii. Kuchunguza mielekeo ya walimu wa shule za msingi Wilayani Igembe Kaskazini kuhusu kauli ya Katiba ya Kenya kwamba serikali itakuza na kuendeleza lugha asilia za watu wa Kenya.
- iv. Kuchunguza mielekeo ya walimu wa shule za msingi Wilayani Igembe Kaskazini kuhusu kauli ya Katiba ya Kenya ya ukuzaji na uendelezaji wa matumizi ya Lugha Ishara ya Kenya na Breli na njia nyingine za mawasiliano na teknolojia zinazoweza kufukiwa na watu wenye ulemavu.

1.3 Maswali Ya Utafiti

Ili kufikia malengo ya hapo juu, utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

- i. Je, walimu wa shule za msingi Wilayani Igembe Kaskazini wana mielekeo gani kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha ya taifa na lugha rasmi nchini Kenya?

- ii. Je, walimu wa shule za msingi Wilayani Igembe Kaskazini wana mielekeo gani kuhusu matumizi ya Kiswahili na Kiingereza kama lugha mbili rasmi shuleni?
- iii. Je, ni ipi mielekeo ya walimu wa shule za msingi Wilayani Igembe Kaskazini kuhusu kauli ya Katiba kwamba serikali itakuza na kuendeleza matumizi ya lugha asilia za Wakenya?
- iv. Je, ni ipi mielekeo ya walimu wa shule za msingi Wilayani Igembe Kaskazini kuhusu kauli ya Katiba kwamba serikali itakuza na kuendeleza matumizi ya Lugha Ishara ya Kenya na Breli na njia nyingine za mawasiliano na teknolojia zinazoweza kufikiwa na watu wenye ulemavu?

1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusu mielekeo ya wanajamii kuhusiana na lugha nchini Kenya. Hata hivyo, tafiti hizi hazijashughulikia mielekeo ya washikadau wa kimsingi, kama vile walimu wa shule za msingi, kuhusu suala la lugha kama linavyoelezwa katika Katiba ya Kenya. Utafiti wa Fink (2005), kwa mfano, unahusu mielekeo kuhusu lugha jijini Nairobi. Katika utafiti huu wake, Fink alichunguza mtindo wa vijana wa uteuzi wa lugha katika muktadha wa jiji la Nairobi. Fink alipata kugundua kwamba mielekeo hasi ya vijana katika jiji la Nairobi kuhusu lugha na tamaduni zao asilia iliwasababisha kupendelea lugha-unde (Sheng') ili kujitambulisha.

Githinji (2008) alishughulikia mielekeo kinzani ya wanajamii kuhusu Sheng' na wazungumzaji wake. Watumizi wa msimbo huu hutoka katika jamiilugha tofautitofauti na huutumia ili kujitambulisha kama kundi moja la kijamii. Kwa hivyo, kwa manufaa ya kujitambulisha, wao huwa na mwelekeo chanya kuhusu msimbo huu ilhali wakati uo huo wao wanauona kama msimbo usio sanifu. Mtaalamu mwingine aliyeshughulikia suala la mielekeo kuhusu lugha ni Mukhwana (2008). Utafiti wake ulichunguza mielekeo ya watu wa miji mitatu (Nairobi,

Mombasa na Kisumu) kuhusu lugha nchini Kenya ili kubainisha hali ya lugha ilivyo katika miji ya Kenya. Mtafiti huyu alipata kugundua kuwa Kiingereza kilienziwa kuliko lugha nyingine mijini kama njia ya kupata ufanisi wa kijamii.

Hapo juu ni mifano tu ya kututanabahisha kuhusu umuhimu wa kuchunguza mielekeo ya watumizi wengine wa lugha kama vile wadau wa kimsingi katika mchakato wa utekelezaji wa sera ya lugha nchini Kenya. Utafiti wetu hivyo basi ulichunguza mielekeo ya walimu wa shule za msingi nchini Kenya kuhusiana na suala la lugha kama linavyoelezwa katika Katiba ya Kenya ya mwaka wa 2010.

Shule ya msingi kama asasi ya kielimu ni mojawapo ya asasi za kimsingi katika ukuzaji na uendelezaji wa matumizi ya lugha nchini Kenya. Isitoshe, walimu wa shule za msingi ndio watekelezaji wa kimsingi wa sera ya lugha kwani darasa huwa ngazi ya mashinani (katika mfumo wa elimu Kenya) ya utekelezaji wa sera ya lugha. Kwa hivyo, mielekeo ya wadau hawa kuhusu suala la lugha ilitufaidi katika utafiti huu kubaini ufahamu, uhusika na ukubalifu wao kuhusu suala hili kama linavyoelezwa katika Katiba ya Kenya ya 2010. Katika utafiti huu, mielekeo ya walimu husika ilikusudiwa kutumika katika kubainisha ushawishi wao katika mchakato wa utekelezaji na vilevile utendakazi wa sera ya lugha nchini Kenya kama inavyojitokeza katika Katiba ya Kenya.

Tulichagua Wilaya ya Igembe Kaskazini kimakusudi ili kuweza kufikia idadi kubwa ya walimu wa shule za msingi katika sehemu za mashambani bila matatizo ya kimawasiliano na kiusafiri. Isitoshe, asilimia kubwa ya walimu wa shule hizi ni wenyeji wa lugha moja asilia, hivyo tungeweza kutathmini mielekeo ya walimu hawa kuhusu lugha yao asilia (Kimeru). Hili lingetuwezesha kufikia lengo letu la (iv) la utafiti huu.

1.5 Upeo Na Mipaka

Utafiti huu ulilenga kuchunguza mielekeo ya walimu wa shule za msingi kama washikadau wa kimsingi katika utekelezaji wa sera ya lugha nchini Kenya. Hata hivyo, tulijibana katika uchunguzi wa mielekeo ya walimu wa shule za msingi katika Wilaya ya Igembe Kaskazini kuhusu suala la lugha kama linavyojitokeza katika Katiba ya Kenya ya mwaka wa 2010.

Walimu walichaguliwa kimakusudi katika utafiti huu kwa sababu wao ni wanajamii walio na weledi wa uteuzi na matumizi ya lugha katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya lugha. Kwa hivyo, mielekeo yao ilitarajiwa kuakisi mielekeo ya washikadau wa kimsingi kuhusu suala hili la lugha nchini Kenya.

Tulichagua walimu wa shule za msingi katika Wilaya ya Igembe Kaskazini kwa sababu wao, kama ilivyo kwa takribani walimu wote wa shule za msingi nchini Kenya, wanafundisha katika wilaya zao za kuzaliwa. Yale wangeyasema kuhusu suala la lugha kama linavyoelezwa katika Katiba ya Kenya yangeakisi mielekeo ya takribani walimu wote wa sehemu za mashambani nchini Kenya. Kama ijulikanavyo, walimu hasa wa shule za msingi ni vielelezo vya kuigwa katika vijiji vingi nchini Kenya. Kwa hivyo, maoni yao kuhusu suala la lugha katika Katiba ya Kenya yalitarajiwa kuakisi kwa kiwango kikubwa, maoni ya walio wengi katika wilaya husika.

1.6 Msingi wa Kinadharia

Dhana ya mielekeo kuhusu lugha inaweza kufafanuliwa kwa kuzingatia mitazamo miwili tofauti: mtazamo wa kiakili na ule wa kitabia (Agheyisi na Fishman, 1970:138). Kwa mujibu wa yaliyomo katika mtazamo wa kiakili, mwelekeo ni hali ya mtu kuwa tayari kutenda jambo fulani ambapo inabidi kuelewa fikra za mhusika kuhusu jambo hilo. Fikra za mtu na mwelekeo wake

kuhusu jambo fulani huchunguzwa kwa kumwuliza maswali yanayolenga kudhihirisha anavyowaza kuhusu jambo husika.

Mtazamo wa kitabia nao huangalia mielekeo kama tabia inayoonekana waziwazi. Kwa mujibu wa mtazamo huu, mwelekeo wa mtu husika kuhusu jambo fulani hubainika kwa kuchunguza tabia anazodhihirisha kuhusiana na jambo hilo.

Mitazamo yote miwili ilituongoza katika utafiti wetu. Hii ni kwa sababu kila mtazamo una mapungufu yake: hakuna unaojitosheleza bila ya kutegemea ule mwingine. Tathmini ya mielekeo ya watafitiwa walengwa iliongozwa na maswali ya moja kwa moja kwa njia ya hojaji na mahojiano yaliyohusisha maoni yao kuhusu majukumu na matumizi ya lugha tofautitofauti kama yanavyojitokeza katika Katiba ya Kenya. Mtafiti vilevile alitazama namna watafitiwa wahusika walivyotumia lugha wakati wa mahojiano na katika mitagusano yao na wenzao na vilevile wanafunzi wao shuleni ili kudhihirisha tabia zao kuhusu lugha mbalimbali.

Mitazamo iliyofafanuliwa hapo juu inazingatia mihimili miwili ya kinadharia: Nadharia ya Kijamiinafsia na Nadharia ya Kijamii. Nadharia hizi mbili zimetufaidi katika kuangazia maana ya dhana ya mielekeo katika ukamilifu wake. Nadharia hizi zimejadiliwa hapa chini na kuonyesha jinsi kila moja inavyohusishwa katika utafiti huu.

1.6.1 Nadharia ya Kijamiinafsia

Mwasisi wa nadharia ya Kijamiinafsia ni Lambert (1963). Kwa mujibu wa Lambert, wazungumzaji hutumia lugha kwa namna tofautitofauti na wasikilizaji wanazingatia mazungumzo hayo kutoa maoni yao kuhusu wazungumzaji. Hapa inakisiwa kuwa maoni ya wasikilizaji hudhihirisha mielekeo yao kuhusu lugha zilizotumiwa na wazungumzaji, sifa bainifu za wazungumzaji, hali zao za kiakili na tabaka lao la kijamii.

Nadharia hii inasisitiza mielekeo inayodhihirishwa na mtu binafsi kuhusu wazungumzaji wengine ndani ya kundi na vilevile nje ya kundi kwa kuzingatia lugha iliyozungumzwa. Mielekeo hii kwa mujibu wa Lambert, huongozwa na sababu za kutaka kujumuishwa katika jamiilugha fulani ili kujitambulisha na vilevile kutaka kupata ufanisi wa kikazi. Hapa wanaopenda kujumuishwa na wale wa jamiilugha yao (kundi-ndani) au jamiilugha ya wengine (kundi-nje) hudhihirisha zaidi mielekeo chanya kuhusu lugha ya jamii husika kuliko wale wanaoongozwa na sababu za kiufanisi maishani (Gardner na Lambert, 1972).

Majukumu muhimu yanayohusishwa na lugha fulani katika jamii pia husababisha watu kuwa na mielekeo fulani kuhusu lugha hiyo (Fishman, 1972:27). Jukumu lililotolewa kutekelezwa na lugha fulani katika jamii hutegemea uungwaji mkono wake na asasi mbalimbali, kama vile shuleni kama lugha ya kufundishia, lugha rasmi au lugha ya taifa (Mukhwana, 2008:31). Ukubalifu wa majukumu ya lugha fulani hivyo basi, hudhihirika kupitia mielekeo ya wanajamii husika. Huu ndio msingi uliotuongoza katika utafiti huu. Majukumu na matumizi ya lugha tofautitofauti yanayoelezwa na Katiba ya Kenya yalitarajiwa kuungwa mkono au kupingwa na wadau watafitiwa, ambao ni walimu wa shule za msingi. Mwitikio wao ulitarajiwa kudhihirisha ushawishi wao katika utekelezaji wa kauli za Katiba ya Kenya zinazohusu suala la lugha nchini Kenya.

1.6.2 Nadharia ya Kijamii

Nadharia ya Kijamii iliasisiwa na Joshua Fishman. Kwa mujibu wa nadharia hii, Fishman (1969) katika Giglioli (1972:45) anaeleza kuwa tabia za wanajamii kuhusu lugha fulani huhusisha, mbali na matumizi ya lugha, pia mielekeo inayodhihirika kuhusu lugha na watumizi wa lugha husika, suala linaloshughulikiwa na viongozi wa kisiasa na kielimu katika sehemu nyingi ulimwenguni.

Fishman (1972:15) anaonyesha jinsi mielekeo kuhusu lugha hutegemea muktadha wake wa kimatumizi. Yaani, kufahamu ni nani anayetumia lugha gani, kwa nani na lini, katika jamiilugha zenye wingilugha. Kwa mujibu wa mtaalamu huyu, tabia kuhusu lugha fulani hutegemea uwanja wa matumizi ya lugha husika na watumizi fulani pamoja na shughuli na mada zinazojadiliwa. Anatumia mtazamo huu katika uchunguzi wake kuainisha nyanja mbalimbali za matumizi ya lugha kama ifutavyo: nyumbani, shuleni, kanisani, kazini, viungani na sehemu za umma mbali na anakoishi mtu. Matumizi ya lugha katika nyanja hizi huongozwa na masiala kama vile uhusiano wa kijamii, mahali walipo wazungumzaji na mada wanayojadili.

Mtazamo wa Kijamii wa Fishman hutumiwa kubainisha uhusiano uliopo baina ya matumizi ya lugha katika mawanda finyu (na mtu kibinafsi) na mawanda mapana (na mtu kama mwanajamii). Kibinafsi, mtu hutumia lugha kujitambua na kujitofautisha na watu wengine. Kama mwanajamii, mtu hutumia lugha kama nyenzo ya kujitambulisha kama mmoja wa wanajamii husika (Hirst, 1986).

Kwa mujibu wa Mukhwana (2008:29), ni muhali kujadili suala la mielekeo kuhusu lugha minghairi ya kuzingatia uhusiano baina ya wazungumzaji na hali au mazingira yanayosababisha mazungumzo hayo. Mtazamo huu ulituongoza vilevile katika utafiti huu unaohusisha uwanja wa elimu (mazingira ya shuleni) kama muktadha wa utafiti wetu.

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Mielekeo ya wanajamii kuhusu lugha yao, ya wengine au lugha kwa jumla husaidia katika kubainisha thamani waliyo nayo wanajamii hao kuhusu lugha husika. Kwa hivyo, utafiti kuhusu mielekeo ya wanajamii, hasa walimu kama washikadau wa kimsingi katika utekelezaji wa sera ya lugha, huelekeza wanajamii katika kufahamu umuhimu unaowekwa na washikadau hao kuhusiana na majukumu na matumizi ya lugha husika.

Tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusu mielekeo, lakini nyingi zimejikita katika mielekeo ya wanafunzi kuhusu masomo, walimu au wanafunzi wengine. Gardner na Lambert (1972), Gardner (1985) na Baker (1992), ni miongoni mwa wataalamu waliotafiti kuhusu mielekeo ya wanafunzi kuhusu ujifunzaji wa lugha shuleni. Kwa mujibu wa Gardner (1985), upataji lugha ya pili hutokea katika muktadha maalum wa kitamaduni na imani ya kijamii kuhusu umuhimu wa kujifunza lugha husika. Umuhimu wa lugha aliyojifunza mwanajamii huendelezwa katika uteuzi wa lugha na matumizi ya lugha husika baada ya kuifahamu. Hivyo basi kuna uhusiano kati ya sifa za kimielekeo na motisha na matumizi ya lugha (Gardner, ibid:174).

Thamani na majukumu yanayotolewa kutekelezwa na lugha fulani huathiri mielekeo ya watu kuhusu lugha hiyo. Vilevile, mielekeo hiyo huathiri tabia za wanajamii katika kujifunza na kuitumia lugha husika (Mohochi, 2011). Utafiti wa Mohochi ulichunguza mielekeo ya wasomi wa Kiswahili na viongozi kuhusu lugha ya Kiswahili. Utafiti huu unatufaidi katika kutanabahi kuwa kutokana na mielekeo yao na ushawishi wao, wasomi kama vile walimu huathiri mielekeo ya wanajamii kuhusu majukumu na matumizi ya lugha husika. Kutokana na utafiti wa mtaalamu huyu, wanajamii hukuzwa katika kuwa na mielekeo hasi au chanya kuhusu lugha tofautitofauti kutoka walipokuwa wanafunzi hadi wanapokufika utu uzima na kupata nafasi za kazi ambapo wengine wao huwa walimu. Mielekeo yao kuhusu lugha itajidhihirisha hata wanaposhikilia majukumu yao ya kikazi, suala linaloshughulikiwa katika utafiti huu.

Tafiti nyingi zimezingatia ukusanyaji wa data uliotumia mbinu ya mlinganuo-fiche. Mbinu hii hutumiwa ambapo wahusika wanaozungumza lugha mbili au zaidi hurekodiwa wakisoma makala kwa lugha tofautitofauti. Baadaye, kanda zilizorekodiwa huchezewa watafitiwa (ambao hawawatambui wasomaji). Baada ya kusikiliza kanda hizo wanaulizwa kutoa maoni yao kuhusu

lugha zilizotumiwa katika usomaji wa makala hizo. Baadhi ya tafiti zilizotumia mbinu hii ni ule uliofanywa na Lambert et al (1960).

Utafiti wa Lambert et al (1960) ulichunguza mielekeo ya wasikilizaji ambao walikuwa wazungumzaji wa Kiingereza na Kifaransa kuhusu lugha hizo mbili jijini Montreal (Canada). Wataalamu hawa walipata kuwa wasikilizaji wa lugha zote mbili waliipa lugha ya Kiingereza hadhi ya juu kuliko ile ya Kifaransa. Mwitikio huu wao ulitokana na sababu za kihistoria ambapo Kiingereza kilithaminiwa na wengi kama lugha ya kupata ufanisi wa kiuchumi na kijamii kuliko lugha nyingine yoyote ile. Kasumba hii imeendelezwa nchini Kenya ambapo, kutoka enzi ya ukoloni, Kiingereza pekee kimepewa jukumu la lugha rasmi hadi mwaka wa 2010 ambapo Kiswahili kilikwezwa kihadhi na kuwa lugha rasmi ya pili. Athari hii ya kihistoria ni mojawapo ya masuala yaliyotusukuma kufanya utafiti wetu, tukichunguza maoni ya walimu wa shule za msingi ili kubaini msimamo wao katika kutekeleza sera ya lugha kama ilivyojitokeza katika Katiba ya Kenya ya mwaka wa 2010.

Watafiti wa baadaye waliotumia mbinu ya mlinganuo-fiche, walipata kwamba wazungumzaji walitathminiwa kulingana na muktadha (usomaji wa matini na usemaji wa kawaida). Hawa ni kama vile Romaine (1980). Wengine ni Cargile na Giles (1997) waliochunguza athari za matumizi ya lafudhi ya kigeni katika kutathmini usemaji wa mzungumzaji wa lugha Kijapani (anayetumia lafudhi ya kigeni). Hata hivyo, tafiti hizi ziliibua mielekeo ya watu kuhusu wazungumzaji wengine na lugha walizotumia kwa kusikiliza tu sauti zao bila kutazama tabia zao kuhusu lugha husika. Utafiti wetu uliegemea maoni ya moja kwa moja na kutathmini mielekeo ya watafitiwa kuhusu majukumu ya lugha na vilevile suala la ukuzaji na uimarishaji wa lugha mbalimbali kama lilivyojitokeza katika Katiba ya Kenya.

Utafiti uliofanywa na Ihemere (2006) kuhusu lugha ya Kiikwerre na Kiingereza cha Kipijini katika jiji la Port Harcourt nchini Nigeria ulitumia mbinu ya mlinganuo-fiche. Kiikwerre hubanwa katika mazungumzo ya kinyumbani ilhali Kiingereza cha Kipijini hutumiwa katika mawanda mapana ya kijamii kama vile shuleni, kazini na katika dini ya Kikristo. Utafiti huu unatubainishia kwamba mielekeo ya watu kuhusu mtu fulani huathiriwa na lugha aizungumzayo pamoja na kiwango chake cha kijamii na kielimu. Utafiti huu wa Ihemere umetuauni si haba katika utafiti wetu kuona matumizi ya lugha na walimu wa shule za msingi yanavyodhihirisha mielekeo waliyo nayo kuhusu lugha hizo na watumizi wake. Kuendelea kuenziwa kwa Kiingereza dhidi ya lugha nyingine nchini Kenya ni dhihirisho linalotosha kuelezea mielekeo chanya waliyonayo walimu husika kuhusu lugha hii dhidi ya lugha rasmi yenzake - Kiswahili.

Mbinu ya mlinganuo-fiche katika kudhihirisha mielekeo ya watu kuhusu lugha ina mapungufu yake. Hii ni kwa sababu msikilizaji anaweza kuishia kupima usomi au usemi na pia msomaji, badala ya lugha husika. Aidha, kama asemavyo Mathooko (2007:88), tathmini inayotumia mbinu hii inaegemea sana upande wa kisaikolojia na kupuuza vipengele vingine vinavyotawala maoni ya wasikilizaji kama vile kidatu cha sauti na toni ya wasomaji. Tofauti na tafiti zilizotumia mbinu hii, utafiti wetu ulitumia mbinu ya hojaji, mahojiano na utazamaji kukusanya data. Mbinu hizi zilitupa data ya moja kwa moja kutoka kwa watafitiwa kwa kuwapa uhuru wa kujieleza, kwa hiyo mtafiti aliweza kufafanua maswali jambo lilosaidia katika kuondoa uwezekano wa utata upande wa maswali. Mbinu tulizotumia zimechangizana kwani ziliegemea mtazamo wa kiakili na kitabia.

Wasomi wengi nchini Kenya wanapendelea kutumia lugha ya Kiingereza kuliko Kiswahili katika miktadha rasmi (Ogola, 1990). Mtaalamu huyu alichunguza mielekeo ya wasomi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili nchini Kenya kwa jumla. Utafiti huu wa Ogola umetufaidi si

haba katika kuona jinsi maoni ya tabaka la waliosoma yalivyo kuhusu Kiswahili nchini Kenya. Walimu ni baadhi ya wasomi hivyo, mielekeo yao kuhusu suala la lugha imeakisi ile ya wasomi wengine nchini Kenya. Hata hivyo, mbali na utafiti wa Ogola ulioangazia mielekeo ya wasomi kwa jumla kuhusu lugha ya Kiswahili, utafiti wetu umeshughulikia walimu wa shule za msingi kuhusu majukumu, ukuzaji na uendelezaji wa lugha tofautitofauti; Kiswahili, Kiingereza, lugha asilia, Lugha Ishara ya Kenya na Breli, kama zilivyoelezwa katika Katiba ya Kenya. Tilitaka kudadisi ikiwa walimu hawa wangedhihirisha tofauti yoyote katika mielekeo yao ya lugha kwa sababu wao ni wadau wa kimsingi katika utekelezaji sera ya lugha nchini Kenya.

Tafiti nyingine zilizotufaidi katika utafiti huu hasa katika kufahamu mbinu za moja kwa moja tulizotumia hazifai kupuuzwa. Utafiti wa Fink (2005) ulichunguza mielekeo ya watu wa jiji la Nairobi kuhusu lugha. Watu wa majijini huwa na lugha tofautitofauti asilia. Vilevile, mtafiti huyu ametumia mbinu ya hojaji kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Daystar kukusanya data. Utafiti wa mtaalamu huyu na ule wa Githinji (2008) ulipata kwamba vijana wa jiji la Nairobi walikuwa na mielekeo chanya kuhusu msimbo uliowatambulisha, Sheng'. Ingawa walijitambulisha kwa msimbo huu utafiti wa Githinji ulibaini kuwa wengi wao hawakuupendelea kwa sababu kukosa usanifu. Githinji anaeleza kwamba wanajamii waweza kuwa na mielekeo inayopendelea lugha inayowatambulisha ilhali wakati huo huo wakawa na mielekeo hasi kuhusu lugha hiyo wanapolinganisha usanifu wake na usanifu wa zile lugha nyingine zinazohusiana nayo (Githinji, ibid: 132).

Utafiti wa Mukhwana (2008) ulipanua ule wa Fink (2005) kwa kuchunguza mielekeo ya watu wa miji mitatu mikuu nchini Kenya ambayo ni Nairobi, Mombasa na Kisumu. Watafiti hawa walipata kwamba katika majiji haya ya Kenya, lugha ya Kiingereza hupendelewa na wengi kama njia ya kupata ajira nzuri na kwa hiyo kuonyesha tabaka ahali la kijamii. Utafiti wa Fink na ule

wa Mukhwana umetufaidi kwa kutubainishia hali ya lugha ilivyo mijini Kenya, kwamba ingawa majukumu ya lugha yamependekezewa, ni jukumu la wadau husika kupanga mikakati ifaayo ili kufaulisha mapendekezo hayo. Hata hivyo, utafiti wa Mukhwana umetathmini mielekeo ya watu wa mijini wenye hadhi na lugha tofautitofauti asilia ilhali utafiti wetu uliangazia mielekeo ya kundi moja la washikadau wa kimsingi (walimu wa shule za msingi) kuhusu suala la lugha kama linavyojitokeza katika Katiba ya Kenya. Wadau hawa wanatoka eneo ambapo walio wengi ni wenyeji wa lugha moja asilia - Kimeru.

Utafiti unaokaribiana na wetu hasa upande wa mbinu za ukusanyaji data ni ule uliofanywa na Kobia na Ndiga (2013). Utafiti huu ulichunguza mielekeo ya wanafunzi wa shule za upili ili kutathmini utekelezaji wa mtalaa wa Kiswahili katika Wilaya ya Igembe Kusini, iliyo jirani na wilaya iliyolengwa katika utafiti wetu. Ingawa utafiti wa wataalamu hawa uliangazia mielekeo ya wanafunzi, umetufaidi katika utafiti huu kutokana na matokeo waliyopata. Utafiti wa wataalamu hawa ulipata kugundua kwamba mielekeo hasi ya walimu kuhusu Kiswahili husababisha mielekeo hasi ya wanafunzi kuhusu lugha hiyo. Wanafunzi hivyo basi huishia kutofaulu katika somo la Kiswahili, hivyo kuendelea kuwa na mielekeo hasi hata baada ya kuhitimu katika masomo ya shule ya upili. Kwa upande mwingine mielekeo chanya ya walimu kuhusu Kiingereza husababisha wanafunzi kupendelea lugha hiyo, na hivyo wao hufanya bidii na kufaulu katika somo la Kiingereza kuliko lile la Kiswahili. Baadhi yao hujiunga na vyuo wanaposomea ualimu. Wawa hawa ndio hufunza baadaye katika shule za msingi, wanamotarajiwa kuhusika katika mchakato wa utekelezaji wa sera ya lugha nchini, suala tuliloangazia katika utafiti wetu.

Mielekeo ya wanajamii kuhusu lugha fulani ni mojawapo ya mambo ambayo yanaweza kuathiri, kwa njia chanya au hasi, ukubalifu wa lugha iliyopendekewa kutekeleza majukumu fulani

(Msanjila et al, 2009:79). Wataalamu hawa wannasema kuwa mielekeo kuhusu lugha fulani hujitokeza zaidi katika jamii ambazo zina wingilugha kama vile Kenya. Walimu wa shule za msingi katika utafiti wetu ni kundi la wanajamii ambalo lina uelewa na ujuzi wa zaidi ya lugha moja (Kiswahili, Kiingereza na Kimeru). Kwa hivyo uchunguzi huu wa mielekeo yao kuhusu lugha hizi ni muhimu ili kudhihirisha ushawishi wao katika utekelezaji wa majukumu yaliyopewa lugha hizi, ukuzaji na uendelezaji wake kama inavyoelezwa katika Katiba ya Kenya.

Mielekeo ya wanajamii kuhusu lugha hutokana na mambo mbalimbali. Mielekeo yao kuhusu lugha inaweza kutokana na mambo kama vile; asasi za elimu, umaarufu wa lugha husika, ulumbi wa wahusika, uwezo wa lugha husika, uana wa wahusika, umri wao, historia ya lugha husika, siasa na utawala katika jamii husika (Mathooko, 2007:93-98). Utafiti huu umechunguza na kugundua kuwa masiala baadhi ya masiala, kama yale yaliyotajwa na Mathooko (2007), yalisababisha mielekeo ya walimu watafitiwa kuhusu lugha tofautitofauti ambazo zinagusiwa na Katiba ya Kenya.

1.8 Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulifanyiwa maktabani na nyanjani. Waliohojiwa katika utafiti huu walikuwa walimu wa shule teule za msingi katika wilaya ya Igembe Kaskazini. Ukusanyaji wa data ulifanywa kwa kuwatembelea walimu hawa katika shule za msingi wanamofundisha ili kuweza kufikia idadi lengwa kwa urahisi.

Kuna takribani shule za msingi 80 wilayani Igembe Kaskazini (data kutoka ofisi ya elimu wilayani Igembe Kaskazini). Ili kuwakilisha walimu katika maeneo yote wilayani Igembe Kaskazini, utafiti huu ulifanyiwa katika maeneo yote 5 ya kielimu, ambayo ni; Antuambui, Kathaanga, Naathu, Ndoleli na Ntunene (data kutoka ofisi ya elimu wilayani Igembe Kaskazini). Kila eneo lilikisiwa kuwa na jumla ya shule 16 (80/5). Asilimia 40% ya shule katika kila eneo

ilifikiwa (shule 6 katika kila eneo). Idadi hii ilitumiwa kwa sababu haingewezekana katika utafiti wowote ule kudadisi na kuhoji kila mtu. Mbinu ya unasibishaji ilitumika kuchagua shule ambazo zingefikiwa katika kila eneo.

Idadi ndogo kabisa ya walimu katika kila darasa ilitarajiwa kuwa mwalimu mmoja. Kwa hivyo, kila shule ilichukuliwa kuwa na idadi ndogo kabisa ya walimu 8. Idadi ya waliowakilisha walimu katika kila shule ni 4 (50%). Kwa hivyo jumla ya walimu waliohusishwa katika utafiti huu ni 120 kutoka maeneo yote 5. Walimu wanne (4) katika kila shule walihojiwa, ambapo tulitembelea shule 6 za kila eneo ($4 \times 6 \times 5 = 120$). Utafiti wetu ulilenga idadi sawa ya walimu baina ya jinsia ya kike na kiume ambapo kila jinsia iliwakilishwa na walimu 60. Walitofautiana kwa tajriba za ufunzaji na vilevile umri wao.

Utafiti huu ulifanywa kwa njia ya maswali ya hojaji, mahojiano na utazamaji wa matendo ya wahojiwa kuhusiana na matumizi ya lugha wakati wa utafiti. Maswali ya hojaji yaliwasilishwa kwa lugha tatu ambazo zilikuwa: Kiswahili, Kimeru na Kiingereza. Hili lilifanywa ili kuepuka upendeleo wa lugha fulani upande wa mtafiti, hali inayoweza kuathiri matokeo ya utafiti. Watafitiwa walihitajika kujaza hojaji kwa lugha waliyoipendelea. Mahojiano yalitumiwa kama njia ya kufafanua maswali ili kuzuia hali ya kuwafunga watafitiwa katika upande wa majibu na vilevile kuondoa uwezekano wa kuwepo kwa utata upande wa maswali.

Hojaji zilijazwa na kukusanywa kwa muda wa wiki tatu. Wakati huo huo utazamaji wa watafitiwa ulifanywa bila ya wao kuhusishwa moja kwa moja na mtafiti alitathmini mielekeo yao kuhusiana na lugha mbalimbali kwa kuzingatia jinsi walivyosikika wakitumia lugha husika walipowasiliana na wanafunzi madarasani, nje ya madarasa na vilevile walivyotagusana na wenzao majilisini. Hili lilitusaidia katika kubaini hali ya lugha ilivyo miongoni mwa walimu katika shule za msingi za mashambani hasa wilayani Igembe Kaskazini.

Vilevile, utafiti huu ulinufaishwa na usomaji ambapo tulidurusu tafiti zilizofanywa kuhusiana na mada yetu. Hili lilifanyiwa maktabani, mtandaoni na kwa kupitia kazi zozote zinazohusu mada yetu ili kufahamu kikamilifu kuhusu mada ya utafiti pamoja na msingi wa kinadharia ulioongoza utafiti huu.

Isitoshe, mashauriano na wataalamu katika idara za lugha yalifanywa ili kupata maelekezo yaliyotufaidi kufaulisha utafiti huu. Tulirejelea wataalamu wanaohusika katika suala la uundaji wa sera ya lugha nchini Kenya ili kupata mwangaza zaidi kuhusu vipengele vya Katiba ya Kenya vinavyogusia suala la lugha nchini Kenya.

1.9 Umuhimu wa Utafiti Huu

Matokeo yaliyopatikana kupitia utafiti huu yatakuwa kirejelewa kwa watafiti wa baadaye kwa sababu ni tafiti chache mno zilizogusia mielekeo ya washikadau wa kimsingi, kama vile walimu wa shule za msingi, kuhusu suala la lugha kama lilivyoelezwa katika Katiba ya Kenya ya mwaka wa 2010.

Utafiti huu pia utawaelekeza washikadau katika sera ya lugha na upangaji lugha kufahamu ni kwa kiwango gani utekelezaji wa kimsingi wa sera ya lugha unavyoshughulikiwa. Huenda mikakati zaidi ikahitajika kupangwa ili kuhimiza uhusika na ushawishi wa washikadau hawa katika mchakato wa utekelezaji au huenda mikakati hiyo isihitajike.

SURA YA PILI

MIELEKEO KUHUSU LUGHA NCHINI KENYA KIHISTORIA NA KATIBA ZA KENYA

2.0 Utangulizi

Jambo la msingi katika sura hii ni kuangalia kihistoria mielekeo ya Wakenya kuhusu lugha mbalimbali nchini Kenya, jambo linalotokana na mielekeo yao kuhusu lugha wanazozifahamu na zile wanazojifunza. Ili kufahamu mielekeo ya Wakenya kama vile walimu kuhusu suala la lugha kama linavyojitokeza katika Katiba ya Kenya, ni muhimu kwanza kuangazia mielekeo ya Wakenya kwa jumla kuhusu majukumu yaliyopewa lugha kutoka enzi ya ukoloni hadi leo nchini Kenya. Mielekeo ya watu huchochea namna wanavyoelekezwa kutumia lugha tofautitofauti.

Utafiti huu unatumia mielekeo ya Wakenya kuhusu lugha kabla ya kuidhinishwa kwa Katiba ya mwaka wa 2010 kama msingi wa kuelewa historia ya sera ya lugha nchini Kenya na vilevile kufahamisha kiini cha mielekeo waliyo wadau kama vile walimu watafitiwa kuhusu lugha tofautitofauti nchini Kenya, kwa kurejelea Katiba hii ya Kenya. Hapa tunaangazia mielekeo iliyotokana na namna Wakenya walivyotumia lugha tofautitofauti kutekeleza majukumu tofautitofauti katika enzi ya utawala wa kikoloni na baada ya ukoloni. Kwa kufanya hivi tunamulika mielekeo ya wadau wa utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya lugha kutokana na hadhi na umuhimu uliopewa lugha za Wakenya mikononi mwa Mwingereza na baada ya Wakenya kupata uhuru.

2.1 Mielekeo Kuhusu Lugha Nchini Kenya Kihistoria

Katika utafiti huu wa kiisimujamii, mielekeo kuhusu majukumu na matumizi ya lugha ni dhana inayohusiana na mabadiliko katika mahusiano ya kijamii miongoni mwa watu wanaowasiliana kutegemea teuzi zao za lugha fulani dhidi ya lugha nyingine kwa manufaa fulani. Mielekeo

hushawishi teuzi na miitikio ya watu kuhusu lugha zao na vilevile kuhusu lugha za wazungumzaji wengine. Ili kuweza kufahamu kiini cha mielekeo ya sasa kuhusu lugha miongoni mwa baadhi ya wadau wa utekelezaji wa sera ya lugha nchini Kenya, ni muhimu kuangazia mielekeo kuhusu lugha nyakati za ukoloni na baada ya ukoloni nchini Kenya, (Kembo - Sure 2002).

2.1.1 Mielekeo Kuhusu lugha Nchini Kenya Katika Enzi ya Ukoloni

Mielekeo ya walimu kuhusu majukumu na matumizi ya lugha tofautitofauti nchini Kenya yanaweza kuathiriwa na kutokea kuwa chanya au hasi kutokana na sera ya lugha iliyokuweco nyakati za ukoloni nchini Kenya. Kuna thamani kubwa inayobebwa na kipindi cha ukoloni nchini Kenya kuhusiana na historia ya sera ya lugha na majukumu yaliyopewa lugha mbalimbali nchini Kenya.

Wamishenari wa awali wa dini ya Kikristo (CMS) wakiongozwa na Dkt J.L. Krapf na Kasisi Steere walijitahidi sana kuendeleza lugha ya Kiswahili kwa kutunga makamusi na vitabu vya sarufi ya Kiswahili. Aidha, waliandika vitabu vya kufunzia Injili katika lugha ya Kiswahili (Chiraghdin na Mnyampala, 1977:54). Kwa wamishenari hawa, walikuwa na mwelekeo kwamba lugha ya Kiswahili ingewawezesha kutagusana na Waafrika na kusambaza elimu na dini ya Kikristo kwa Wakenya Waafrika.

Wamishenari wa baadaye nao walikuwa na mwelekeo hasi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili. Mwelekeo huu ulitokana na sababu kwamba Kiswahili kilihusishwa na lugha ya Kiarabu na kwa hivyo dini ya Kiislamu, iliyokuwa imeenezwa na Waarabu pwani ya Afrika Mashariki kabla ya kuja kwa Wazungu. Jambo hili lilipelekea kutiliwa mkazo kwa matumizi ya lugha za kienyeji katika kueneza dini ya Kikristo nchini Kenya. Wamishenari hao walikipinga Kiswahili kwa kuamini kuwa kilikuwa lahaja ya Kiarabu (Mbaabu 1991:8).

Kupitia Tume ya Elimu Afrika Mashariki (*Tume ya Beecher* ya 1942-1948), lugha ya Kiswahili ilipigwa marufuku katika shughuli za kimishenari za kueneza dini ya Kikristo kwa Waafrika (Mazrui 1978:228). Mwelekeo huu ulisababishwa na ukweli kwamba Waswahili wengi walikuwa Waislamu na lugha ya Kiswahili ilikuwa imeomba baadhi ya msamiati kutoka lugha ya Kiarabu. Hivyo basi wamishenari walikihusisha Kiswahili na dini ya Kiislamu.

Wamishenari walianzisha shule ambamo Kiingereza kingefundishwa kama somo na Kiswahili kingetumiwa kufundishia masomo mengine. Walipendekeza lugha za kiasili ziweze kutumika kufundishia katika madarasa ya mwanzo mwanzo kisha Kiswahili kifuatie (taz. Gorman 1974:405, Mbaabu, 1996:5-6).

Karne ya kumi na tisa ndiyo iliyokuwa msingi wa uundaji wa sera ya lugha Kenya katika enzi ya ukoloni. Hata hivyo, ilikuwa vigumu kwa wamishenari kutumia lugha za kiasili kuendeleza shughuli za kueneza dini ya Kikristo na pia elimu. Kwa mfano, Kongamano la Muungano wa Wamishenari (The United Missionary Conference) la mwaka wa 1901 lilishindwa kutumia lugha hizi. Kwa hivyo, lugha iliyowafaa katika shughuli hizi mbili ikawa Kiswahili (Muthiani 1986).

Kanuni za maandishi na matumizi ya lugha ya Kiswahili zilianza kupangwa kwa mchango wa wamishenari kama vile Askofu Steere, Ludwig Krapf na John Rebmann, ambao walifanya uchunguzi kuhusu lugha ya Kiswahili hatua kwa hatua (Mbaabu 1991:8). Palianzishwa asasi za kimishenari ambazo zilikuwa vituo vya kibiashara, kielimu na vilevile kimatibabu (taz. Mukhwana, 2008). Msamiati wa Kiswahili uliendelezwa kwa kasi hasa katika asasi hizo. Ingawa hapo awali istilahi za Kiswahili zilikuwa zikifafanuliwa na wenyeji wa lugha hii, mielekeo chanya waliyokuwa nayo wamishenari Wakristo kuhusu lugha ya Kiswahili iliwawezesha kuchangia katika ukuzaji wa msamiati wa lugha hii, ingawa wao walikuwa wageni. Kutokana na mwelekeo chanya wa wamishenari kuhusu lugha ya Kiswahili, makamusi na vitabu vingi vya

sarufi ya Kiswahili viliandikwa. Hili liliwawezesha wamishenari hawa kuendeleza matumizi ya lugha hii ya Kiswahili, hivyo kuinuliwa kwa hadhi yake.

Licha ya mchango wa wamishenari wa kukuza na kuendeleza Kiswahili, kulikuwa na mapungufu katika uendelezaji wa lugha ya Kiswahili, jambo lililosababisha mielekeo hasi miongoni mwa Waswahili na wamishenari wa jamii tofautofauti kwa sababu ya maendeleo tofautitofauti ya Kiswahili na usanifishaji upya. Wamishenari walitofautiana kuhusu lahaja bora ya kutumiwa katika usanifishaji wa Kiswahili. Isitoshe, sajili iliyohusishwa ilikuwa ya dini ya Kikristo, hivyo Waswahili wengi waliokuwa Waislamu wakawa na mielekeo hasi kuhusu Kiswahili (Mbaabu, 1991:9-19).

Mielekeo ya serikali ya Waingereza ilitofautiana mara kwa mara na ile ya wamishenari kuhusu lugha mwafaka za kutumiwa kutekelezea majukumu ya kielimu. Japo wamishenari walipendelea lugha za kienyeji zitumiwe, mara nyingi watawala nao walisisitiza matumizi ya lugha ya Kiingereza. Kwa kufanya hivi, watawala hawakunua kuwa lugha itumike katika kufanikisha mawasiliano tu, bali pia koloni yao ijitegemee kiuchumi na wao wenyewe kujistawisha. Walipendelea Kiingereza kitumiwe ili waendeleze pia ukoloni wa kilugha.

Serikali ya kikoloni haikuwa na sera maalumu kuhusu lugha. Baadhi ya watawala, kama vile Mkuu wa Mkoa wa Pwani wa wakati huo, C. Hobley, walipendelea lugha za Kiingereza na Kiswahili zisomeshe (Gorman 1974:406). Mkurugenzi wa Elimu J.R. Orr naye alikuwa na mwelekeo kwamba ni muhimu kusomesha lugha za kienyeji. Kwake, kusomesha Kiswahili kulikuwa kupoteza wakati, kwani mwelekeo wake ulikuwa kwamba lugha ya Kiswahili haikuwa na manufaa yoyote ya kielimu. Kwa hivyo, mnamo Septemba 1919, alitoa agizo kwamba Kiingereza kisomeshe katika shule zote zilizopewa ruzuku na serikali. Madai kama haya kuhusu lugha na tamaduni za Wakenya yaliwaelekeza Wakenya kufikiri na kuamini kwamba

Kiingereza ndiyo lugha bora na inayoendeleza utamaduni bora kuliko lugha za kienyeji (Jones, 1925:8).

Wakati wa ukoloni, lugha ya Kiingereza ilionewa fahari na Wakenya walio wengi. Wazazi wengine walipendelea watoto wao wafundishwe kwa lugha ya Kiingereza kwa kuamini kuwa wangepanikiwa kupata ajira nzuri. Mwelekeo chanya kuhusu lugha ya Kiingereza ulitokana na imani ya wazazi hawa, kwamba ingewawezesha kujinua kiuchumi kupitia matumizi ya lugha hii. Lugha ilitumiwa kama nyenzo ya kupitishia elimu kwa Wakenya. Baadaye kamati ya kuishauri serikali kuhusu lugha za kutumiwa kutekelezea majukumu ya kielimu iliundwa.

Tume ya Phelps-Stokes ya 1924 ilipotembelea Kenya ililalamikia hali ya sera ya lugha iliyohitilafiana nchini Kenya kati ya wamishenari na maafisa wa serikali. Tume hii ilipendekeza lugha kadhaa za Kiafrika (kama vile Kiswahili, Kikikuyu, Kidholuo, Kiluhya na Kinandi) zisanifishwe na zitumike katika elimu. Baadaye Mkurugenzi wa Elimu aligundua kuwa ilikuwa ghali kuchapisha vitabu vya kutosha kwa lugha za kienyeji. Kwa hivyo, alisema kwamba Kiswahili kitumike kufundishia katika shule za Kiafrika (Gorman, ibid: 412).

Baada ya Vita vya Pili vya Dunia, wakoloni walilegeza upendeleo wao wa Kiswahili kwa mwelekeo kwamba lugha hii ingekuwa kizuizi kati ya Kiingereza na lugha za kienyeji. Waingereza walikuwa na nia ya kukisambaza Kiingereza kwa Waafrika, hivyo walikiona Kiswahili kama kilichoweza kuleta upinzani kwa sababu kingewaunganisha Waafrika baada ya vita. Lililofuatia mwelekeo huu ni kwamba Kiswahili kiliwekwa pamoja na lugha nyingine za kienyeji. Baadaye kulikuwa na tofauti katika silabasi kwa sababu ya mafunzo kutolewa kwa lugha tofautitofauti - Kiingereza, Kiswahili na lugha asilia. Kwa hivyo, Wakenya hawakupata fursa sawa za kielimu (Mukhwana 2008:57). Hali hii iliwapa Wakenya wa wakati huo kuwa na mwelekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili.

Sera ya kukuza lugha ya Kiingereza na kudunisha Kiswahili ilipata msingi imara baada ya ripoti ya *Tume ya Beecher* ya mwaka wa 1942 na ile ya 1949. Kwa mujibu wa yaliyomo katika ripoti hizi, msisitizo ulistahili kuwekwa katika ufundishaji wa lugha za kienyeji na lugha ya Kiingereza kuchukua nafasi ya lugha ya Kiswahili. Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika elimu yalipingwa na mnamo mwaka wa 1949 tume hii ikapendekeza lugha ishirini za kienyeji zitumiwe kufundishia shule za vijijini. Kwa hali hii, inatarajiwa kuwa mielekeo ya Wakenya kuhusu lugha ya Kiswahili ingekuwa hasi.

Matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia yalibanwa kwenye shule za mijini pekee. Wakenya walivyozidi kufundishwa kwa lugha ya Kiingereza ndivyo walivyozidi kujifunza utamaduni wa Waingereza na kudharau utamaduni wao wa Kiafrika. Waliendelea kuiga na kuienzi mienendo ya Waingereza kwa imani ya kujiinua kiuchumi na kisiasa, kinyume na wale wasiofahamu Kiingereza. Kupitia elimu hivyo basi, Wakenya wakawa na mwelekeo chanya kuhusu Kiingereza na kuzichukia lugha zao za kienyeji.

Kutoka mwaka wa 1949, lugha za kienyeji zilifundishwa na malengo ya miaka mitatu ya kwanza shuleni yakaelezwa katika mtaala kuwa ni kujua kusoma na kuandika katika lugha za kienyeji. Sehemu ya utekelezaji wa ripoti ya Beecher ya 1942 ilikuwa kukifundisha Kiingereza kutoka darasa la tatu na kuenda juu. Kufikia 1952, Kiingereza kilifanywa kuwa lugha ya lazima ya kufundishia na kutahini mwishoni mwa ngazi ya masomo ya shule ya msingi. Kiswahili kilifanywa kuwa somo lisilotahiniwa katika shule za msingi (Mbaabu, 1991: 84). Hii ni kumaanisha kuwa kulipandwa chembe za mielekeo hasi kuhusu lugha Kiswahili na lugha nyingine asilia kwa Wakenya kutoka kwa wakuza mitaala.

Kiswahili na lugha nyingine za kienyeji zilitumiwa na watawala wa kikoloni ili kuwatenganisha Waafrika na kuwapumbaza kama mpango wa kimakusudi wa kuwagawanya ili wakoloni

waweze kuwatawala kwa urahisi. Sera ya lugha chini ya utawala wa kikoloni ilihakikisha kuendelea kwa mipaka ya lugha iliyowagawa Waafrika na kuwatenganisha na wananchi wenzao (Gorman, 1974: 426). Lugha za kienyeji Kenya zilifikiriwa kuwa duni ilhali Kiingereza kilipewa hadhi ya juu.

Kabla ya uhuru nchini Kenya, lugha ya Kiswahili ilitumiwa katika mawasiliano kati ya mabwana Waingereza na watumishi wao waliokuwa Waafrika. Hapa, mwelekeo uliojitokeza kuhusu lugha ulikuwa kwamba lugha ya Kiswahili haikuwa na hadhi ya juu. Kiswahili kilionekana kama lugha ya wananchi wa kawaida wasiokuwa na jukumu muhimu katika utawala. Kiingereza nacho kilichukuliwa kama lugha ya kifahari na ya watu wenye hadhi ya juu katika jamii. Hii ilisababisha Kiingereza nchini Kenya kuonekana kama lugha ya kifahari na daraja la kupata elimu bora kwa waliobahatika kupata elimu katika lugha hii (Mukhwana 2008:60). Hata baada ya ukoloni, Wakenya wengi wameonyesha upendeleo kwa matumizi ya Kiingereza kwa sababu kimeenziwa kutoka nyakati za ukoloni. Hili ni dhihirisho la mielekeo chanya kuhusu lugha hii ambayo imekuwa lugha rasmi kutoka kuja kwa wakoloni hadi leo.

Nchini Kenya, wakati wa ukoloni, Kiswahili na lugha nyingine za kienyeji zilitumika kama lugha za mawasiliano kati ya watawala na watawaliwa na miongoni mwa wenyeji wa lugha hizi. Kiingereza kilichukuliwa na Wakenya kama njia ya kusaidia kupata madaraka wakati wa ukoloni.

Kwa mujibu wa Chiraghdin na Mnyampala (1977), Wakenya walikuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za kienyeji kwa sababu kadhaa:

- i. Lugha ya Kiingereza Kenya ilihusishwa na tabaka la wasomi na watawala ambao walienziwa kuliko wale wasiosoma kwa lugha hii.

- ii. Kiingereza kilichukuliwa kama daraja la kupata elimu na kujiinua kijamii, kiuchumi na kisiasa. Hii ina maana kuwa nchini Kenya, lugha hii ilihusishwa na kazi nzuri na vyeo muhimu katika utawala, kanisani na katika biashara. Vyeo hivi vilikuwa vya Wakenya waliokuwa wamesoma.
- iii. Wakenya walikuwa wameelekezwa na wakoloni kuchukulia lugha zao za kienyeji kama zilizokosa ustaarabu, hivyo hazikustahili kutumika katika elimu. Hili lilichochea mielekeo hasi kuhusu lugha hizo.
- iv. Lugha za kienyeji kama vile Kiswahili zilisanifishwa na Wazungu ambao walikuwa wa asili za Kiingereza na Kijerumani. Jambo hili lilisababisha utata kwa wenyeji wa lugha na lahaja tofautitofauti, wakazona lugha zao kama zenye ugumu kusoma kwa sababu ya tofauti katika othografia, sarufi na matamshi.
- v. Wakuu wa shule na walimu waliwazuia wanafunzi dhidi ya kuwasiliana kwa lugha zao asilia. Waliokiuka sheria hii (waliotumia lugha zao asilia shuleni) waliadhibiwa kwa kubebeshwa mabango yalichoandikwa kwa mfano: *“I am a fool”*, au *“I don’t know English”* Yaani *“Mimi ni mjinga”*, au *“Sijui Kiingereza”* (wa Thiong’o 1986:11). Adhabu hii ilikuwa ya kufedhehesha kwa wanafunzi kama hawa, hivyo wakawa wamechukia kuwasiliana kwa lugha zao za asilia wakiwa shuleni. Matokeo yake ni kuwa Wakenya walipendelea kuwasiliana kwa lugha ya Kiingereza ili wasifedheheshwe kwa kuzungumza lugha zao za kienyeji. Hili linadhihirisha mielekeo hasi ya Wakenya dhidi ya lugha zao za kienyeji na mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiingereza wakati wa ukoloni. Mielekeo hii ilisababishwa na mfumo wa elimu uliokuwepo wakati huo.

2.1.2 Mielekeo Kuhusu Lugha Nchini Kenya Baada ya Ukoloni

Ingawa Wakenya wengi walikuwa na mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiingereza wakati wa ukoloni, baadaye Wakenya wasomi waliitumia lugha hii kuanzisha mapinduzi. Kupitia masomo

kwa lugha ya Kiingereza, Wakenya waligundua hila za utawala wa kikoloni. Walianza kutafuta juhudi ya kuwaunganisha na wenzao kama jamii yenye maadili sawa kinyume na walivyochukuliwa na wakoloni.

Wakenya waliopata elimu walipata ari ya kujitawala na kusahau walichofaidi kutokana na kuenzi lugha ya Waingereza. Kwa hivyo wao walitafuta uhuru wa kilugha ili waweze kujipatia uhuru wa kisiasa. Kiswahili kilichukuliwa kama lugha ya kuwaunganisha wakenya na kupigania uhuru wao. Aliyekuwa Rais wa kwanza wa Kenya, hayati Jomo Kenyatta, alitangaza Kiswahili kuwa lugha ya taifa baada ya uhuru. Hili lililenga kuchochea Wakenya kuwa na mwelekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili kama kiunganishi na kitambulisho cha jamii ya Wakenya. Hata hivyo, hakukuwa na sera au sheria iliyoandikwa kufafanua jinsi majukumu hayo ya lugha nchini Kenya yalivyofaa kutekelezwa kupitia sekta ya elimu (Kibiwott 2006:3).

Taifa huru la Kenya lilirithi asasi za kielimu, kisiasa, kiuchuni na kisheria kutoka katika kipindi cha ukoloni. Kupitia urithi wa asasi hizi, Kenya ilijipata ikirithi pia lugha ya watawala wa kikoloni, Kiingereza, kama lugha yake rasmi. Baada ya Kenya kupata uhuru, lugha ya Kiingereza ilichukua nafasi ya lugha rasmi na Kiswahili kikawa lugha ya taifa la Kenya. Kaida za kikoloni za kuchunguza namna ambavyo sera za lugha zingeundwa hazikuvunjwa ingawa Kenya ilipata uhuru. Mtazamo wa kikoloni uliendelezwa kwa kukipa Kiingereza hadhi ya juu na kukitweza Kiswahili na lugha nyingine za kiasili. Kiingereza kiliendelea kuwa lugha rasmi katika Kenya huru (Mbaabu 1996: 58). Mwelekeo uliojidhihirisha dhidi ya lugha za kiasili na Kiswahili ni hasi huku Wakenya wakidhihirisha mwelekeo chanya kuhusu Kiingereza.

Kama ilivyokuwa katika enzi ya ukoloni, tume na kamati mbalimbali ziliteuliwa na serikali huru ili kuchunguza na kupendekeza mabadiliko yaliyostahili katika sera za lugha nchini Kenya. Kila

tume au kamati ilikuwa na mwelekeo tofauti kuhusiana na lugha zipi na kwa vipi zilifaa kutumika katika mfumo wa elimu.

Tume ya Elimu Kenya, iliyoongozwa na Prof. Ominde S.H wa Chuo Kikuu cha Nairobi, ilitoa ripoti mwaka wa 1964 ikipendekeza matumizi ya Kiingereza kama lugha ya kufundishia kuanzia darasa la kwanza katika shule za msingi. Kiswahili nacho kilipendekezwa kufundishwe kama somo la lazima katika shule za msingi kwa sababu kilitumiwa kama lugha yenye umuhimu wa kuwaunganisha Wakenya na kuwa ni *Lingua Franca* ya kimaeneo. Pendekezo la tume hii linadhihirisha mwelekeo chanya kuhusu jukumu la Kiingereza kama lugha rasmi katika mfumo wa elimu Kenya, huku Kiswahili kikichukuliwa kama lugha yenye jukumu la kuwatambulisha Wakenya (kama lugha ya taifa).

Pendekezo la Tume ya Ominde lilitupiliwa mbali kwa madai kwamba lugha ya Kiswahili ingekuwa ngeni kwa watoto wa jamii za Kiasia na zile zisizo za Kibantu kwa madai kuwa ingekuwa vigumu kuwafunza watoto lugha mbili zilizo ngeni. Aidha, maoni ya wananchi ya kukitaka Kiswahili kiwe lugha ya kufundishia katika shule za upili yalipuuzwa na Tume ya Ominde. Mwelekeo wa tume hii ni kwamba ingekuwa ghali kutafsiri vitabu hadi lugha ya Kiswahili, shughuli waliyodai kuwa ingekuwa matumizi mabaya ya pesa za umma. Mwelekeo huo ulichangia katika kudumaza maendeleo ya lugha hii.

Ripoti ya Kamati ya Ukufunzi iliyoongozwa na mwenyekiti wa Baraza la Utumishi wa Umma, Bwana W. N Wamalwa mwaka wa 1971 ilipendekeza kuwa lugha ya Kiswahili ikuzwe na kuendelezwa. Hili lilizingatiwa na serikali kwa muda kisha likapuuzwa. Kamati hii ilipendekeza Kiswahili kutumiwa kama lugha ya taifa. Ili kupata ufasaha katika lugha ya Kiswahili kwa wafanyikazi wote wa umma, kamati hii ilipendekeza kwamba kozi shadidi zianzishwe katika vyuo vinavyowaandaa wafanyikazi wa utumishi wa umma. Vyuo hivyo ni kama vile Taasisi ya

Utawala Kenya (KIA) na Taasisi ya Ukufunzi wa Serikali (GTI) (Ripoti ya Wamalwa 1971). Serikali iliyatekeleza mapendekezo haya kwa muda na wakayatupilia mbali baadaye. Hili lilionyesha mwelekeo hasi wa serikali na mawakala wake kwa kupuuza umuhimu unaoambatana na ukuzaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa. Hili ni suala ambalo ni kiini cha mielekeo waliyo nayo baadhi ya wadau wa utekelezaji wa sera ya lugha kama vile walimu nchini Kenya hata nyakati za leo.

Kamati ya Kitaifa kuhusu malengo ya sera ya elimu iliyoongozwa na Bw. P.J Gachathi, ilipendekeza kwamba lugha tawala za maeneo ambamo shule zimejengwa zitumiwe kuwafundishia wanafunzi katika miaka mitatu ya kwanza shuleni. Lugha ya Kiswahili ilipendekezwa itumike kufundishia katika shule za mijini. Kiingereza kilipendekezwa kitumike kufundishia katika shule za miji ambamo mna mchanganyiko wa asili ya watu. Hii ilimaanisha kuwa aidha Kiingereza, Kiswahili au lugha za kienyeji zingetumika kufundishia katika darasa la kwanza hadi la tatu nchini Kenya, kutegemea ilikokuwa shule husika. Pendekezo jingine la kamati hii ni kwamba lugha ya Kiingereza ifundishwe kama somo kutoka darasa la kwanza na kuanzia darasa la nne Kiingereza kichukue nafasi ya lugha za kienyeji na Kiswahili kama nyenzo ya kufundishia (Chimera 1998).

Lugha ya Kiswahili ilipendekezwa kuwa somo la lazima na la kutahiniwa mwishoni mwa masomo ya shule ya msingi. Vilevile Kiswahili kilipendekezwa kifundishwe na kutahiniwa kama somo la lazima katika kiwango cha shule ya upili. Mapendekezo haya yalidhihirisha mielekeo chanya ya wadau sera ya lugha iliyokitambua Kiswahili kama lugha muhimu kupitia mfumo wa elimu. Hata hivyo, Kiswahili kilipewa vipindi vitatu kwa wiki, ilhali Kiingereza kilipata vipindi vinane. Aidha, Kiswahili kilipendekezwa kianze kufundishwa katika daraja ya vyuo vikuu na walimu wa Kiswahili waandaliwe zaidi jambo lililolengwa kuwashawishi walimu na wanafunzi

kuwa na mielekeo chanya kuhusu Kiswahili kwa kukionea umuhimu kama walivyokiona Kiingereza.

Licha ya mtazamo wa tume ya Gachathi, pendekezo la kukifanya Kiswahili kuwa somo la lazima na la kutahiniwa katika shule za msingi na ya upili halikutekelezwa hadi mwaka wa 1985, serikali ilipoanzisha mfumo mpya wa elimu wa 8-4-4. Kutotiliwa maanani kwa kukifanya Kiswahili somo la lazima na la kutahiniwa kuliwafanya wanafunzi wengi kuwa na mwelekeo hasi kuhusu lugha hii na kuipuuza kama lugha isiyo na manufaa maishani.

Tume iliyoongozwa na Dkt. C. B. Mackay (1981) ilipendekeza sera ya lugha iliyopendelea na kuhimili maendeleo ya lugha ya Kiswahili. Tume hii pia ilipendekeza kufundishwa kwa Kiswahili katika kiwango cha vyo vikiu. Ilipendekeza kuwa katika chuo kikuu kilichonuiwa kuanzishwa na serikali (cha Moi), kuanzishwe kitengo cha Lugha za Kiafrika kilichofaa kujumuisha Kiswahili na lugha nyingine za Wakenya katika Kitivo cha Mtalaa wa Kijamii, Utamaduni na Maendeleo. Kiswahili kilipendekezwa kuwa somo la lazima katika chuo hicho kipyaa, kwa kuhoji kuwa kulikuwa na wanafunzi wengi waliohitimu elimu ya chuo kikuu lakini hawangeweza kuwasiliana kwa Kiswahili - lugha ya taifa. Kufuatia pendekezo hili Idara ya Kiswahili ilianzishwa chuoni humo mwaka wa 1987. Aidha, walipendekeza Kiswahili kijumuishwe katika Somo la Mawasiliano kwa wanafunzi wote wa mwaka wa kwanza.

Kwa kutazama mapendekezo ya *Ripoti ya Mackay*, tunatanabahishwa kuhusu jukumu la lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa na tume hii ilinuia kujenga msingi imara wa kukikuza na kukiendeleza Kiswahili nchini Kenya. Hatua ya serikali ya kukubali pendekezo la kuanzisha mfumo wa elimu wa 8-4-4 ambapo lugha ya Kiswahili ilifanywa somo la lazima na kutahiniwa katika shule za msingi na sekondari ni muhimu katika ukuzaji wa lugha hii. Jambo hili limewahamasisha wengi kuwa na mwelekeo chanya na kukionea fahari Kiswahili na hata

wataalamu kuchapisha vitabu mbalimbali kwa lugha hii ya Kiswahili. Hata hivyo, tume hii ilipendekeza kuwa lugha ya Kiingereza ibakie kama lugha ya kufundishia. Lugha za kienyeji nazo zilipendekezwa zitumike kufundishia darasa ya chini katika shule za msingi, lakini katika maeneo ambamo hili lingewezekana (Njoroge, 1990). Wakenya, wakiwemo walimu, walidhihirisha mielekeo hasi dhidi ya Kiswahili na lugha nyingine za kienyeji. Lugha za Kiafrika zilichukiwa shuleni na kuzitumia badala ya Kiingereza kulichukuliwa kama ujinga (wa Thiong'o, 1986:11).

Mnamo Aprili, 1970 Mpango wa Chama Tawala cha KANU wa kukifanya Kiswahili lugha rasmi uliibuliwa. Wakenya wote wangezungeza lugha hii wakati wowote na yeyote katika muktadha wowote, rasmi au usio rasmi. Shughuli zote za serikali zilifaa zierendeshwe kwa Kiswahili. Hata waliowania ubunge, udiwani au teuzi zozote serikalini walifaa kuongea Kiswahili kizuri na ambao wangehutubia hadhara kwa dakika zisizopungua kumi. Raia wa nje ya nchi waliotafuta uraia wa Kenya walihitajika kuonyesha, kwa maandishi au mazungumzo, uwezo wa kutumia Kiswahili. Kushindwa kufanya hivyo kungepelekea yeye kupoteza uraia wake wa Kikenya.

Kiswahili kilipendekezwa kipewe kipaumbele kuliko Kiingereza katika shule za msingi na za upili. Serikali iliahidi kuanzisha na kufadhili kozi na vituo vya kufundishia, kusoma na kukuza lugha ya Kiswahili katika mikoa yote na pia kujenga taasisi moja kuu ya kitaifa. Hili lililenga kushawishi watu kuwa na mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, kauli hizo zilikuwa za kisiasa tu na serikali haikujitolea kufuatilia pendekezo hilo, jambo lililosababisha Wakenya kuendelea kuwa na mielekeo hasi dhidi ya Kiswahili (Mbaabu, 1996:132-134).

Nchini Kenya, kulichapishwa taarifa za Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa kila baada ya miaka mitano baada ya Kenya kupata uhuru. Hata hivyo, ni taarifa mbili tu ambazo ziliangazia suala la lugha.

Mpango wa maendeleo wa 1979-83 ulitaja kuanzishwa kwa Taasisi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Sehemu ya taarifa ya mpango huo inasema:

“chuo kitaanzisha mtalaa wa Kiswahili ili kusaidia utoaji wa maandishi ya kutosha na makala nyingine za kielimu kwa ufundishaji wa Kiswahili katika shule. Uwezekano wa kuanzisha Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili utachunguzwa wakati wa kipindi cha mpango huu,” (Mpango wa Maendeleo 1979-83: 166).

Dondoo hili linadokeza jaribio la serikali la kuanzisha Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili nchini Kenya. Mbaabu (1996: 134) anaeleza kuwa taarifa ya mpango huu ilipochapishwa, Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Nairobi kwa ushirikiano na Idara ya Isimu na Lugha katika Chuo Kikuu cha Kenyatta ilianza kuandaa makadirio ya mahitaji ya taasisi hiyo: vifaa na majukumu.

Katika taarifa ya Mpango wa Maendeleo wa 1984-88, serikali ilitangaza kuwa ingefadhili utekelezaji wa elimu ya kujifunza kusoma na kuandika kwa watu wazima. Hili lingefanyika kupitia mafunzo kuhusu maisha ya kifamilia na afya, uraia mwema na maendeleo ya vijijini. Mipango hii inatarajiwa kuwa kishawishi cha mielekeo chanya kuhusu Kiswahili miongoni mwa Wakenya, wakiwemo walimu. Hata hivyo, serikali haikufuatilia mipango hii na mwishowe haikuanzisha taasisi iliyokusudiwa kuongoza katika utafiti, maandishi, uundaji wa msamiati na hivyo ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, mielekeo iliyokidunisha Kiswahili na kukitukuza Kiingereza ilibakia miongoni mwa Wakenya.

2.2 Katiba za Kenya

2.2.1 Toleo lililorekebishwa, 1969 na 1992

Toleo la Katiba ya awali ni msingi unaotubainishia kuwa, kinyume nayo, katiba ya sasa imepiga hatua kubwa katika kushughulikia suala la lugha nchini Kenya. Katiba ya sasa imetaja majukumu mbalimbali yanayoambatishwa kwenye lugha tofautitofauti za Wakenya na kuonyesha kuwa kuna juhudi za serikali ya Kenya za kulinda, kukuza na kuendeleza matumizi ya lugha hizo.

Katiba ya awali iligusia tu sifa za mtu ambaye alinuia kuwania ubunge, lugha za kutumiwa bungeni na yaliyohitajika kuzingatiwa na mtu aliyetafuta uraia wa Kenya. Sehemu ya 34 (c) ya katiba ya awali imetaja kwamba, mtu anayewania ubunge anahitajika kuwa mwenye ustadi katika lugha ya Kiingereza na ya Kiswahili. Sehemu ya 53(1) imetangaza lugha rasmi za bunge kuwa Kiingereza na Kiswahili. Ili kujiandikisha kama raia wa Kenya, mtu alihitajika kumridhisha waziri husika kuwa ana ufahamu toshelevu wa Kiswahili (sehemu ya 93: e). Hata hivyo, Kiingereza ndicho kilichohitajika kutumika kuandikia na kunukuu kila mswada wa sheria ya Bunge, maamuzi ya kifedha na marekebisho yoyote ya stakabadhi zilizotajwa. Hili linaonyesha kwamba hakukuwa na usawa baina ya lugha hizi mbili za Kiingereza na Kiswahili. Mwelekeo unaobainishwa hapa kuhusu Kiswahili ni hasi ilhali ule unaohusu Kiingereza ni chanya.

Kama tulivyoeleza awali, ukweli ni kwamba sera ya lugha ya wakoloni iliendelea kuonekana ikiendelezwa na serikali hata baada ya Kenya kupata uhuru. Hata hivyo, kuna ishara kwamba wakati mwingine serikali ilibadili msimamo na kuzipa lugha za kienyeji, kikiwemo Kiswahili, umuhimu ila tu ari hii ilionekana kufifia kwa kupuuzwa baada ya muda mfupi. Hii ilifanya lugha

husika, kama vile Kiswahili, zisipige hatua katika uendelezaji na ukuzaji wake, jambo linalodhihirisha mwelekeo hasi dhidi ya lugha za kienyeji.

Ingawa kuna fursa nzuri ya kuzitilia maanani lugha za Wakenya katika katiba ya Kenya ya 2010, sharti serikali ijitolee kwa kutenga rasilmali za kifedha na iwe na mipango maalum ya utekelezaji ili kufanikisha kauli za katiba ya sasa. Bila kuyanya haya, mielekeo ya Wakenya kuhusu lugha, wakiwemo walimu, itazidi kuwa kama ilivyokuwa hapo awali, kabla ya kupitishwa kwa Katiba ya mwaka wa 2010.

2.2.2 Katiba ya Kenya ya Mwaka wa 2010

Katiba inayotumika sasa nchini Kenya ilirekebisha, ikapendekezwa na kupitishwa na Wakenya mnamo Agosti 4, 2010. Katiba hii imeleta matumaini mapya kuhusu suala la lugha nchini Kenya. Kauli za Katiba hii zinazohusu suala la lugha nchini Kenya zinaakisi sera ya lugha inayotambua hali ya wingilugha ambayo haikutambuliwa katika katiba ya zamani.

Kwa mujibu wa yaliyomo katika Katiba ya Kenya (Sura ya 2, Ibara ya 7), lugha ya Kiswahili kama lugha mojawapo ya lugha za kienyeji na lugha ya taifa, imekwezwa kihadhi na kuwa pia lugha rasmi sambamba na lugha ya Kiingereza. Aidha, serikali imenuia kutunza, kukuza na kuendeleza matumizi ya lugha asilia za Wakenya. Lugha Ishara ya Kenya na Breli zimetambuliwa kisheria kama njia za mawasiliano miongoni mwa watu walio na changamoto za kimaumbile (Sura ya 4, ibara ya 54). Hali hizi zinatupa kufikiri kuwa mielekeo ya Wakenya hasa wadau wa mashinani kuhusu lugha mbalimbali itabadilika na hili ndilo hasa lengo la kufanya utafiti huu.

2.2.2.1 Sera ya Lugha Nchini Kenya kwa Mujibu wa Katiba ya Kenya (2010)

Kenya ni nchi iliyo na zaidi ya lugha 40 zinazozungumzwa na watu wa makabila tofautitofauti (Abdulaziz, 1982). Maelekezo ya Katiba ya Kenya ya 2010 yanaangazia hali hii ya wingilugha, nchini Kenya. Kuteuliwa kwa lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa na kuongezewa jukumu la kuwa lugha rasmi sambamba na Kiingereza kunadhihirisha kuwa ofisi zote za kiserikali na vilevile zile zinazohudumia umma zinafaa kuzingatia kauli hii ya Katiba. Hii ina maana kuwa lugha hizi mbili zitatumika katika mawasiliano rasmi kati ya maafisa wa umma na wananchi katika kiwango cha kitaifa na vilevile majimboni. Mazungumzo rasmi hivyo basi yanaweza kufanywa kwa lugha rasmi, Lugha Ishara ya Kenya, Breli au lugha asilia inayopendelewa na hadhira lengwa hasa katika majimbo husika.

Jitihada za kutoa nyenzo za kutafsiri zinafaa kufanywa inapowezekana (Jamhuri ya Kenya, 2013:28). Ili kuhakikisha utekelezaji wa sera inayohusishwa na lugha rasmi, serikali ya Kenya haina budi kubuni mikakati ya kuhakikisha kuwa Wakenya wamebadili mtindo wa kutumia Kiingereza katika ofisi za serikali na asasi za elimu. Hili litakiwezesha Kiswahili kutumika katika miktadha sawia na Kiingereza (Jamhuri ya Kenya, 2013:25). Mielekeo chanya kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi inatarajiwa kudhihirika miongoni mwa Wakenya ikiwa mikakati mwafaka itabuniwa.

Katiba ya Kenya (2010) imetaja kwamba matumizi ya lugha asilia za Wakenya yatalindwa, kukuzwa na kuendelezwa. Kauli hii inazingatia haki za matumizi ya lugha kama zinavyoelezwa katika Azimio-Bia la Haki za Matumizi ya Lugha (UNESCO, 1998). Kwa kuangazia suala la haki za matumizi ya lugha, serikali ya Kenya haina budi kubuni njia za kuhakikisha kuwa kila Mkenya amehudumiwa kwa kutumia lugha anayoiielewa inapohitajika (Jamhuri ya Kenya,

2013:12). Jambo hili litavutia mielekeo chanya kuhusu lugha zao asilia, jambo ambalo halikutokea kabla ya kuidhinishwa kwa Katiba ya mwaka wa 2010.

Isitoshe, serikali ya Kenya inahitajika kubuni njia za kuhakikisha kwamba elimu ya msingi katika madarasa ya mwanzo mwanzo imetolewa kwa lugha tawala ya eneo la shule husika (Jamhuri ya Kenya, 2013:23). Ili kukuza lugha ya Taifa – Kiswahili, Serikali inafaa ianzishe kitengo cha kufunzia na kutahini Kiswahili kama lugha ya Kigeni. Hili litawawezesha raia wa kigeni nchini kutumia Kiswahili katika kufanya kazi au tafiti zao kokote nchini. Swali ni je, watekelezaji wa kimsingi wa sera ya lugha kama vile walimu wana mielekeo gani kuhusu ukuzaji wa lugha hizi tukijua kwamba wengi wamerithi mielekeo iliyokuwepo kutoka enzi ya ukoloni? Hili ndilo suala kuu linalotafitiwa katika tasnifu hii.

Kauli kwamba serikali ya Kenya imenuia kukuza na kuendeleza matumizi ya Lugha Ishara ya Kenya na Breli ni dhahirisho kwamba lugha ya Wakenya wenye changamoto za kimaumbile kuhusiana na lugha yanalindwa katika ngazi ya kitaifa. Swali tunalojiuliza ni je, wadau katika sekta kama ya elimu wana mwelekeo gani kuhusu miundo mbalimbali ya mawasiliano inayotumiwa na watu wenye changamoto za kimaumbile? Swali letu linatokana na ufahamu kwamba Wakenya wanafaa kuwa na motisha ya kujifunza na kutumia Lugha Ishara ya Kenya ili kufaulisha mawasiliano na hivyo, ushirikiano wa Wakenya katika ujenzi wa taifa moja. Walimu, kwa mfano, wanapotagusana na wanafunzi wenye changamoto za kusikia, wanafaa kuwa na mielekeo inayokubali matumizi ya Lugha Ishara kama lugha ya kuwafundishia. Hii ni kwa sababu hii ndiyo lugha ya kwanza ya wanafunzi hawa (Adoyo, 2002:89). Utafiti huu ulilenga kuchunguza mielekeo inayodhahirishwa na walimu wa shule za msingi kuhusu suala hili la matumizi ya Lugha Ishara ya Kenya na Breli.

Kutokana na kauli tulizozijadili hapo juu kuhusiana na suala la lugha katika Katiba ya Kenya ya 2010, swali tunalouliza ni je, ni upi mwelekeo wa walimu wa shule za msingi kama wadau wa kimsingi kuhusu kauli hizi za Katiba zinazohusiana na matumizi ya lugha nchini Kenya? Wadau hawa wana mielekeo inayokubali au isiyokubali kauli kama hizi za Katiba ya Kenya? Mielekeo waliyo nayo walimu wa shule za msingi nchini Kenya inachochewa na masiala yapi?

Katika sura zinazofuata tunaangazia mielekeo ya walimu wa shule za msingi wilayani Igembe Kaskazini ili kupata kujibu maswali hayo yahasuyo suala muhimu la lugha kama linavyoelezwa katika Katiba ya Kenya ya 2010.

2.3 Hitimisho

Katika sura hii ya pili, tumejadili suala la mielekeo ya Wakenya kuhusu matumizi ya lugha nchini Kenya kutoka enzi ya ukoloni hadi sasa. Tumeangazia nafasi ya serikali ya kikoloni katika kuathiri namna ambavyo watu wameitikia lugha tofautitofauti nchini Kenya. Kwa kusema hivi tuna matarajio kwamba matumizi ya lugha fulani katika kutekeleza majukumu fulani yameshawishi Wakenya, kwa njia chanya au hasi, kuwa na mielekeo fulani kuhusu lugha husika.

Kiingereza kimeenziwa kama lugha rasmi nchini Kenya kutoka enzi ya utawala wa mkoloni. Wakenya walikienzi Kiingereza kwa sababu lugha hii ilichukuliwa kama daraja la kupata ajira bora na kujiinua kiuchumi. Lugha za Kienyeji zilichukuliwa kama lugha za mawasiliano ya kikabila nchini Kenya. Kwa hivyo, lugha za kienyeji hazikufaa kutumika katika elimu ya juu isipokuwa Kiswahili kilichofunzwa kama somo la lazima katika shule za msingi na sekondari. Wakenya wengi waliishia kuwa na mielekeo chanya kuhusu Kiingereza na mielekeo hasi kuhusu lugha zao asilia. Wakenya wenye changamoto za kimaumbile wameshughulikiwa katika Katiba ya Kenya ya mwaka wa 2010.

Ingawa hali ya lugha katika utawala wa kikoloni iliathiri mielekeo waliyokuwa nayo Wakenya hata baada ya uhuru, Katiba ya Kenya iliyopitishwa mnamo Agosti, 2010 imeleta matumaini mapya kwa sababu ya serikali kuzitambua na kunuia kukuza na kuendeleza matumizi ya lugha tofautitofauti za Wakenya. Hata hivyo, hofu iliyopo ni kwamba huenda kauli hizi zipuuzwe kama ilivyokuwa awali na Wakenya waendeleo kupata mielekeo ya jadi kuhusu lugha mbalimbali.

Katika sura inayofuata tunashughulikia mielekeo ya baadhi ya walimu kama wadau wa kimsingi kuhusu suala hili la mielekeo kuhusu suala la lugha kama lijitokezavyo katika Katiba ya Kenya ya mwaka wa 2010.

SURA YA TATU

MATOKEO NA UCHANGANUZI WA MATOKEO YA UTAFITI

3.0 Utangulizi

Katika sura hii mielekeo ya walimu wa shule za msingi wilayani Igembe Kaskazini kuhusu lugha ya Kiswahili na Kiingereza imejadiliwa. Mielekeo hii imejadiliwa kwa kuangazia majukumu ya lugha hizi kama yanavyoelezwa katika Katiba ya Kenya. Kwanza, tulichunguza mielekeo ya walimu hawa kuhusu kauli ya Katiba inayoeleza kwamba lugha ya taifa la Kenya ni Kiswahili. Mielekeo kuhusu kauli hii ya Katiba ilichunguzwa ili kubaini mwikio wa walimu husika kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha iliyo au isiyo na uwezo wa kutekeleza jukumu la lugha ya taifa nchini Kenya.

Isitoshe, mielekeo ya walimu wa shule za msingi kuhusu kauli ya Katiba ya Kenya kwamba Kiswahili kitumike kama lugha rasmi sambamba na lugha ya Kiingereza nchini Kenya imejadiliwa. Kwa kufanya hivi tulilenga kubaini nafasi ya kila moja ya lugha hizi mbili katika utekelezaji wa majukumu yazo katika miktadha tofautitofauti rasmi nchini Kenya. Mojawapo ya matumizi rasmi ya lugha hii ni katika elimu ya msingi ambapo walimu ndio wadau wa kutekeleza na kuhimiza matumizi ya lugha hii.

Mielekeo ya watafitiwa kuhusu lugha asilia ya Kimeru imejadiliwa. Aidha, mielekeo ya walimu waliohojiwa kuhusu kauli ya Katiba ya Kenya kuhusu ukuzaji na uimarishaji wa lugha asilia, Lugha Ishara ya Kenya na Breli imeangaziwa.

Kiini cha utafiti huu ni ukinzani wa kimielekeo unaoweza kuwapo miongoni mwa wadau wa utekelezaji wa sera ya lugha katika nchi yenye wingilugha kama ilivyo Kenya (taz. Amolloh, 2012). Kwa hiyo, mielekeo ya walimu wa shule za msingi kuhusu lugha hudhihirisha hali ya

wadau hawa ya kukubali au kutokubali kutekeleza majukumu ya lugha husika katika miktadha lengwa. Kwa hivyo matokeo ya uchunguzi kama huu wetu yatakuwa maelekezo muhimu katika kupanga mchakato wa utekelezaji wa matumizi lengwa ya lugha husika.

3.1 Matokeo ya Utafiti

Uchunguzi huu ulilenga watafitiwa 120. Hojaji zote zilijazwa na kurejeshwa kwa mtafiti. Ili kupata mielekeo ya walimu wa shule za msingi kuhusu lugha ya Kiswahili, Kiingereza na Kimeru kwa jumla, watafitiwa waliulizwa, kwa mazungumzo, kuhusu lugha waliyoipendelea kutumia katika kujaza hojaji ya utafiti. Walimu 45 (asilimia 37.5% ya watafitiwa wote) walipendelea kujaza hojaji zilizoandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Walimu 75 (asilimia 62.5%) walichagua kujaza hojaji zilizoandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Hakukuwa na mhojiwa aliyependelea kujaza hojaji iliyoandikwa kwa lugha ya Kimeru.

Kwa upande wa umri, asilimia 80% (walimu 24 kutoka kwa 30) ya wenye umri wa kati ya miaka 20 na 30 walipendelea kutumia lugha ya Kiswahili kujazia hojaji ilhali walimu 6 kutoka kwa 30 (asilimia 20%) walichagua kujaza hojaji za Kiingereza. Asilimia 32.8% (walimu 21 kutoka kwa 64) ya wenye umri wa kati ya miaka 31 na 40 walipendelea kutumia lugha ya Kiswahili kujazia hojaji ilhali walimu 43 kutoka kwa 64 (asilimia 67.2%) walichagua kujaza hojaji zilizoandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Hakuna mwalimu mwenye umri wa zaidi ya miaka 40 aliyechagua kujaza hojaji kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Walimu wote 26 (asilimia 100%) katika kiwango hiki cha umri walipendelea kujaza hojaji za lugha ya Kiingereza. Jedwali lifuatalo linadhihirisha matokeo hayo:

Kielelezo 1: Upendeleo kwa Lugha ya Kujazia Hojaji - Kiumri

UMRI (MIAKA)	20 - 30	31 – 40	41 – 50	Zaidi ya 50	JUMLA
LUGHA					
Kiswahili	24 (80%)	21 (32.8%)	0 (%)	0 (%)	45 (37.5%)
Kiingereza	6 (20%)	43 (67.2%)	26 (100%)	0 (%)	75 (62.5%)
Kimeru	0 (0%)	0 (0%)	0 (0%)	0 (0%)	0 (0%)
JUMLA	30 (100%)	64 (100%)	26 (100%)	0 (0%)	120 (100%)

Tulipoangazia suala la jinsia, idadi sawa ya walimu baina ya jinsia zote mbili ilitafitiwa. Kila jinsia hivyo basi, iliwakilishwa na walimu 60 kwa 120 (asilimia 50%). Katika jinsia ya kike, asilimia 22% ya walimu hao (Walimu 13 kwa 60) walipendelea kutumia lugha ya Kiswahili kujazia hojaji ilhali asilimia 78% (walimu 47 kwa 60) walipendelea kujaza hojaji kwa kutumia lugha ya Kiingereza. Kwa upande wa jinsia ya kiume, asilimia 53% ya walimu hao (Walimu 32 kwa 60) walipendelea kutumia lugha ya Kiswahili kujazia hojaji ilhali asilimia 47% (walimu 28 kwa 60) walipendelea kujaza hojaji kwa kutumia lugha ya Kiingereza. Jedwali lifuatalo linadhihirisha matokeo hayo:

Kielelezo 2: Upendeleo kwa Lugha ya Kujazia Hojaji - Kijinsia

JINSIA	Kike	Kiume	JUMLA
LUGHA			
Kiswahili	13 (22%)	32 (53%)	45 (37.5%)
Kiingereza	47 (78%)	28 (47%)	75 (62.5%)
Kimeru	0 (0%)	0 (0%)	0 (0%)
JUMLA	60 (100%)	60 (100%)	120 (100%)

Tajriba ya kikazi kwa watafitiwa ilitofautiana kutoka miaka 2 hadi miaka 18. Wengi wa watafitiwa (asilimia 22.5%) walikuwa na tajriba ya miaka 8 na walikuwa jumla ya walimu 27. Asilimia 77.5% ya watafitiwa (walimu 93) ilichukuliwa na tajriba ya ufundishaji.

3.2 Mielekeo kuhusu Majukumu ya Kiswahili

Uchanganuzi wa matokeo ya utafiti huu umefanywa kwa kuzingatia malengo mahsusi ya utafiti.

3.2.1 Mielekeo Kuhusu Kiswahili Kama Lugha ya Taifa Kenya

Mielekeo ya walimu wa shule za msingi kuhusu dhima ya Kiswahili kama lugha ya taifa nchini Kenya ilichunguzwa ambapo watafitiwa waliulizwa kutoa maoni yao kuhusu kauli ya katiba ya Kenya kwamba Kiswahili kitumike kama lugha ya taifa Kenya. Zaidi ya asilimia 80% ya watafitiwa wote walionyesha mielekeo chanya iliyopendelea matumizi ya lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa la Kenya. Hata hivyo kuna watafitiwa wachache (waliopungua asilimia 20%) walioipinga kauli hii ya katiba ya Katiba ya Kenya.

3.2.2 Mielekeo Kuhusu Kiswahili Kama Lugha Rasmi

Kutokana na matokeo ya utafiti huu asilimia kubwa ya watafitiwa walionyesha mielekeo chanya kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi katika mianda rasmi nchini Kenya na hii ni kama vile katika shule za msingi nchini Kenya. Watafitiwa 74 kutoka kwa 120 ni idadi iliyowakilisha asilimia 61.7% ya watafitiwa ambao walipendelea matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi nchini Kenya, hasa katika kufundishia katika shule za msingi. Wengi miongoni mwa watafitiwa walioonyesha mielekeo chanya kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi ni walimu wenye umri kati ya miaka 31 na 40. Hata hivyo kuna ugunduzi katika utafiti huu kwamba wale waliouona umuhimu wa jukumu la Kiswahili kama lugha rasmi ya kufundishia hawakupendelea kutumia lugha hiyo katika mazungumzo rasmi. Japo ufundishaji ni mwanda rasmi, hali hii ilitushangaza na kwa hiyo ipo haja ya utafiti zaidi kufanywa ili kubaini ni kwa nini walimu hawa walikuwa na mwelekeo kama huu.

Kwa kuangazia tajriba ya watafitiwa katika uwanja wa kufundisha tunapata kwamba walimu wenye tajriba ndefu walionyesha mielekeo chanya kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi. Tunataka tukumbushe hapa kwamba ingawa wengi wa watafitiwa katika kiwango hiki cha umri hawakupendelea kujaza hojaji kwa Kiswahili wao walipendelea hadhi rasmi iliyopewa lugha ya Kiswahili nchini Kenya. Upo uwezekano kwamba maoni kama haya yanatokana na ukweli kwamba taifa jirani la Tanzania limetumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia katika shule za msingi na vyuo vya walimu kwa mafanikio makubwa (Mtafitiwa namba 43).

Utafiti huu unaonyesha uhusiano wa kiasi kati ya mielekeo kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi na suala la jinsia. Hata hivyo, uhusiano huu si mkubwa. Watafitiwa wa jinsia ya kiume, kinyume na wenzao wa kike, wana mielekeo inayopendelea zaidi matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi nchini Kenya. Tajriba ya watafitiwa haikuathiri upendeleo wa Kiswahili kama lugha rasmi.

Hii ni kwa sababu tajriba zimeenea kutoka miaka 2 hadi 10. Kutokana na mwelekeo huu wa wanawake kuhusu Kiingereza, ile dhana kwamba wanajamii wa kike katika jamii za Kiafrika hupendelea vitu vya kigeni inatiliwa mkazo. Si ajabu kwamba walimu wa kiume waliohojiwa walikipendelea zaidi Kimeru na Kiswahili kuliko walivyokienzi Kiingereza.

3.3 Mielekeo Kuhusu Matumizi ya Lugha ya Kiingereza

Kutokana na utafiti huu, mielekeo kuhusu lugha ya Kiingereza ilichunguzwa kwa kuzingatia maelezo ya Katiba ya Kenya kwamba Kiingereza ni mojawapo ya lugha rasmi nchini Kenya. Katiba hii pia imeeleza kwamba serikali itakuza na kulinda lugha tofautitofauti za Wakenya. Kiingereza ni mojawapo ya lugha za Wakenya na hutumiwa katika miktadha mbalimbali ya kijamii hasa miktadha iliyo rasmi.

3.3.1 Mielekeo Kuhusu Kiingereza kama Lugha Rasmi


Kama idadi kubwa ya watafitiwa ilivyodhihirisha kuwa ipo mielekeo chanya kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi nchini Kenya, vivyo hivyo ndivyo ilivyokuwa tulipochunguza mielekeo kuhusu Kiingereza kama lugha rasmi. Watafitiwa waliulizwa ikiwa kuna manufaa ya kutumia lugha Kiingereza kama lugha rasmi nchini Kenya. Swali hili lililenga kubainisha ikiwa watafitiwa walienzi lugha ya Kiingereza kama lugha rasmi ingawa imepewa hadhi rasmi sambamba na Kiswahili. Asilimia kubwa (88.5%), iliyowakilishwa na watafitiwa 105, iliafikiana na hoja kwamba kuna umuhimu wa kuendelea kutumia lugha ya Kiingereza katika mianda rasmi nchini Kenya. Hata hivyo watafitiwa hawa walieleza kwamba waunda sera na wapangaji lugha wafaa kubuni mbinu mwafaka za kuwawezesha kudhibiti utekelezaji wa jukumu rasmi la lugha hizi mbili bila kuonyesha upendeleo kwa lugha mojawapo. Hii ni kwa sababu miaka minne baada ya kuidhinishwa kwa Katiba hii ya Kenya majukumu na matumizi ya

lugha nchini Kenya yamekuwa kama yalivyokuwa kabla ya kupitishwa kwa Katiba hii (Mukhwana, 2013).

Watafitiwa walipoulizwa kuhusu lugha waliyoionea fahari wakati wa mazungumzo rasmi ikilinganishwa na Kiswahili, zaidi ya asilimia 80% walichagua mazungumzo kwa lugha ya Kiingereza, dhidi ya waliopungua asilimia 20% ambao walichagua Kiswahili. Utafiti huu uligundua kwamba ingawa idadi kubwa ya watafitiwa walikubali kwamba kuna umuhimu wa kutumia Kiingereza kama lugha rasmi, wengine wao walichagua kutumia Kiswahili kama lugha waliyoionea fahari kutekeleza mazungumzo rasmi. Kwa watafitiwa hawa, lugha ya Kiswahili ni lugha iliyo karibu kimuundo na lugha yao asilia ya Kimeru. Lugha zote mbili ni za Kibantu zilizo katika tapo la lugha za Kibantu za Mashariki kwa mujibu wa tafiti za wataalamu kama vile Greenberg (1963) na Whiteley (1974).

Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kwamba kuna uhusiano baina ya suala la umri na upendeleo katika kutumia lugha kufanyia mazungumzo rasmi. Sampuli katika utafiti huu iligawanywa katika makundi manne kiumri, kila moja likiwakilisha rika fulani. Watafitiwa wa umri wa kutoka miaka 41 na zaidi, wote walionyesha upendeleo wa kutumia Kiingereza katika kufanya mazungumzo rasmi. Wengi wa watafitiwa wa umri wa kati ya miaka 31 na 40 (zaidi ya asilimia 60%) walipendelea kutumia Kiingereza katika mazungumzo rasmi kuliko Kiswahili. Asilimia ndogo sana ya watafitiwa wa umri kati ya miaka 20 - 30 (waliopungua asilimia 20%) walikionea fahari Kiingereza kama lugha ya kufanya mazungumzo rasmi. Chati ifuatayo inaakisi matokeo hayo:

Kielelezo 3: Matumimizi ya Kiingereza Katika Mazungumzo Rasmi - Kiumri



Jambo jingine lililojitokeza katika utafiti huu ni lile la uhusiano baina ya upendeleo wa matumizi ya lugha fulani na jinsia. Watafitiwa wengi wa kike kuliko wa kiume walipendelea kufanya mazungumzo rasmi kwa kutumia lugha ya Kiingereza. Utafiti ulipata kugundua kwamba asilimia 78% ya watafitiwa wa kike walipendelea mazungumzo rasmi kwa lugha ya Kiingereza. Asilimia 47% ya watafitiwa wa kiume walipendelea mazungumzo rasmi kwa lugha ya Kiingereza. Hali hii imewakilishwa kwenye jedwali kama ifuatavyo:

Kielelezo 4: Matumizi ya Kiingereza Katika Mazungumzo Rasmi - Kijinsia


JINSIA	Chanya	Hasi	JUMLA
Kike	47 (78%)	13 (22%)	60 (100%)
Kiume	28 (47%)	32 (53%)	60 (100%)
JUMLA	75 (62.5%)	45 (37.5%)	120 (100%)

3.4 Mielekeo Kuhusu Lugha Asilia (Kimeru)

Watafitiwa walipoulizwa kuchagua lugha ya kujazia hojaji, hakukuwa na mtafitiwa aliyejaza hojaji kwa kutumia lugha ya Kimeru. Hata hivyo, matokeo ya utafiti yalidhihirisha kwamba asilimia 75.8% (walimu 91 kutoka kwa 120) waliyaonea fahari mazungumzo ya nyumbani kwa lugha yao asilia ambayo ni Kimeru. Asilimia 24.2% ya watafitiwa (walimu 29 kutoka kwa 120) walionyesha mielekeo hasi na isiyoyaonea fahari mazungumzo ya nyumbani kwa lugha asilia ambayo ni Kimeru. Watafitiwa waliodhihirisha mielekeo hasi kuhusu matumizi ya lugha ya Kimeru, waliwakilishwa na walimu wenye umri wa kati ya miaka 20 – 31.

Kwa watafitiwa hawa, Kuzungumza lugha ya Kimeru ni kukutukuza ukabila nchini Kenya. Aidha, kwao lugha inayofaa kusesitizwa ni ile itakayowafaidi watoto wao katika kupita mitihani shuleni, kama vile Kiingereza kikichanganywa na Kiswahili. Matokeo haya yanaakisiwa katika chati ifuatayo

Kielelezo 5: Matumizi ya Kimeru katika Mazungumzo ya Nyumbani




Matokeo ya utafiti wetu yalidhihirisha kwamba hakuna tofauti kubwa ya upendeleo iliyodhihirika kati ya jinsia ya kike na kiume. Vilevile, walio wengi katika vikundi vyote vya kiumri vilivyotafitiwa waliyaonea fahari mazungumzo ya kinyumbani kwa lugha asilia. Hii

inaonyesha kwamba suala la jinsia na vilevile umri halikuathiri mielekeo ya watafitiwa katika suala la matumizi ya lugha nyumbani.

Tulipochunguza mielekeo ya watafitiwa kuhusu kauli ya ukuzaji na uendelezaji wa matumizi ya lugha yao asilia (Kimeru), idadi ya waliodhihirisha mielekeo chanya kuhusu kauli hii ilikuwa asilimia 58.3% (walimu 70 kutoka kwa 120). Nayo idadi iliyopinga kauli hii ilikuwa asilimia 41.7% (walimu 50 kutoka kwa 120). Matokeo haya yameakisiwa katika chati ifuatayo:

Kielelezo 6: Ukuzaji na Uendelezaji wa Lugha Asilia (Kimeru)



3.5 Mielekeo Kuhusu Ukuzaji na Uendelezaji wa Matumizi ya Lugha Ishara na Breli

Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha mielekeo chanya ya watafitiwa kuhusu kauli ya Katiba ya Kenya kwamba serikali itakuza na kuendeleza matumizi ya Lugha Ishara ya Kenya na Breli. Watafitiwa walipongeza juhudi za serikali ya Kenya kwa kujumuisha mafunzo ya lugha hizi katika mfumo wa elimu. Baadhi ya watafitiwa wanatoka katika familia zilizo na watu wenye hali za ulemavu wa ama kuona au kusikia na kwa hiyo, ili kupunguza unyanyapaa unaokwenda na hali hizi, wanaiona serikali kama iliyofanya jambo la busara. Hata hivyo, watafitiwa walieleza

kuwa juhudi zaidi zinahitajika upande wa serikali ili kuwawezesha walemavu wengi kufikia huduma kwa lugha husika.

3.6 Hitimisho

Katika sura hii ya tatu tumewasilisha matokeo ya utafiti wetu kuhusu mielekeo ya walimu kuhusiana na suala la lugha kama lilivyoielezwa katika Katiba ya Kenya. Matokeo yameonyesha kwamba lugha ya Kiingereza inapendelewa zaidi nchini Kenya kuliko ile ya Kiswahili. Vilevile, lugha ya Kimeru haikupendelewa na yeyote katika kujazia hojaji. Kwa hiyo, lugha asilia ya Kimeru inachukuliwa kama lugha ya mawasiliano ya nyumbani tu. Walimu waliohojiwa walikuwa na mielekeo chanya kuhusu dhima ya Kiswahili kama lugha ya taifa na vilevile kama lugha rasmi nchini Kenya. Vilevile, utafiti huu umebainisha kuwa lugha ya Kiingereza imeenziwa kama lugha rasmi nchini Kenya.

Ingawa matokeo yalidhihirisha kuwa lugha ya Kimeru haikuchaguliwa kujazia hojaji, watafitiwa waliokuwa wengi waliionea fahari lugha hii kwa matumizi ya nyumbani. Vilevile, walimu waliohojiwa waliafikiana pakubwa na kauli ya kuikuza na kuiendeleza lugha yao asilia na pia Lugha Ishara ya Kenya, Breli na miundo mingine ya mawasiliano inayoweza kufikiwa na walemavu.

Katika sura ifuatayo, tumejadili masiala yanayosababisha mielekeo mbalimbali kuhusu lugha kama ilivyojitokeza katika utafiti.

SURA YA NNE

MASIALA YANAYOSABABISHA MIELEKEO YA WALIMU WA SHULE ZA MSINGI KUHUSU SUALA LA LUGHA KAMA LILIVYOELEZWA KATIKA KATIBA YA KENYA

4.0 Utangulizi

Mielekeo ya wanajamii kuhusu lugha fulani huchochewa na masiala tofautitofauti. Kama ilivyodhihirishwa kupitia maoni ya wahojiwa, miongoni mwa masiala hayo kuna yale ya kihistoria, kiisimu, kijamii na kiuchumi. Katika sura hii, tumefafanua masiala yaliyosababisha mielekeo tofautitofauti miongoni mwa walimu wa shule za msingi wilayani Igembe Kaskazini kuhusu kauli zinazohusu suala la lugha kama linavyojitokeza katika Katiba ya Kenya ya mwaka wa 2010. Masiala haya yanatoa mwangaza kwa wadau katika upangaji lugha na uundaji wa sera ya lugha kuhusu mikakati inayohitajika kubuniwa ili kudhibiti hali ya lugha nchini Kenya.

Katika sehemu zinazofuatia, masiala yanayosababisha mielekeo ya watafitiwa kuhusu uteuzi na matumizi ya kila moja ya lugha za Wakenya zilizogusiwa na Katiba ya Kenya yamejadiliwa.

4.1 Masiala Yanayosababisha Mielekeo Kuhusu Kiswahili

Kutokana na utafiti huu, watafitiwa walidhihirisha mielekeo iliyoongozwa na masiala ya kihistoria, kijamii, kiisimu na kiuchumi. Watafitiwa waliodhihirisha mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa na rasmi nchini Kenya walidhihirisha kwamba upendeleo wao kuhusu majukumu haya ya lugha hii ulitokana na kutaka kujihusisha na wenzao kama jamii moja ya Wakenya. Hii inamaanisha kwamba suala la utambulisho wa kijamii na uzalendo kupitia matumizi ya Kiswahili ni muhimu. Suala hili limejitokeza pale tulipata watafitiwa wakieleza kwamba Kiswahili ni lugha inayoleta utangamano wa kitaifa miongoni mwa Wakenya.

Watafitiwa waliokipendelea Kiswahili kitumike kama lugha rasmi waliegemea katika lengo la kuikua lugha hii kama lugha ya taifa itakayowaunganisha Wakenya kama jamii moja. Hata hivyo, wengi wa watafitiwa hawa walieleza hofu yao kwamba Kiswahili hakijapewa nafasi ya kukua kwa hivyo walipendekeza lugha hii itumike katika kufundishia wanafunzi wa madarasa ya mwanzomwanzo katika mfumo wa elimu ya shule za msingi Kenya. Kwa kufunziwa katika madarasa ya mwanzomwanzo, misingi imara ya Kiswahili itakitwa miongoni mwa Wakenya walio wengi. Aidha, vitabu zaidi vya kufundishia vilipendekezwa vichapishwe kwa lugha ya Kiswahili ili kueneza uelewa wa lugha hii kwa wengi nchini Kenya. Wengine walipendekeza ukufunzi wa ualimu katika lugha ya Kiswahili ili kukuza na kuendeleza lugha hii miongoni mwa washika-dau wakuu na muhimu.

Utafiti huu ulipata watafitiwa wachache walioonyesha kutopendelea matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa sababu za kiisimu. Mifano ya hawa ni wale watafitiwa waliokuwa na maoni potovu kwamba Kiswahili ni lugha ya Kibantu na kwa hivyo, hueleweka kwa urahisi na Wakenya wengi na walio Wabantu. Kwa maoni ya walimu hao watafitiwa, kufundishia kwa lugha ya Kiswahili ni muhali kwa sababu, kwa maoni yao, Kiswahili hukosa istilahi fulani fulani za kisayansi na kiteknolojia ambazo hupatikana katika lugha ya Kiingereza. Wengine wao walidhihirisha madai potovu kwamba msamiati wa Kiswahili ni mgumu na unaobadilikabadilika kila wakati. Kwa kubadilikabadilika hivi, watafitiwa hawa walidai kuwa hakuwezi kuwa na upatanifu kati ya wanaofundisha na wale wanaofundishwa kwa kutumia lugha hii.

Zaidi ya asilimia 60% ya watafitiwa ilichagua kutumia lugha ya Kiingereza badala ya Kiswahili kujazia hojaji. Hofu yao ilidhihirika walipoeleza kwamba ilikuwa vigumu kujieleza kwa lugha ya Kiswahili. Sababu za kihistoria katika mfumo wa elimu zilitolewa kama kisababishi cha matatizo hayo ya kiisimu. Walimu hao walipitia mfumo wa zamani wa elimu ambapo lugha ya

Kiswahili haikuchukuliwa kama somo muhimu kwa Wakenya kama ilivyochukuliwa lugha ya Kiingereza. Kiswahili hakikutahiniwa katika ngazi ya shule za msingi na ilipokuja kwenye ngazi ya shule za sekondari, lugha hii haikuhesabiwa kama somo muhimu lililompa mwanafunzi fursa ya kujiunga na chuo kikuu kama ilivyo sasa. Kwa sababu hiyo, watafitiwa hao hawakupata fursa ya kuumudu msamiati wa Kiswahili ili kuyaonea fahari matumizi ya lugha hiyo katika kujieleza. Kwa maoni ya watafitiwa, hili lilitokana na hali ya Wakenya kutawaliwa kilugha na wakoloni jambo walilorithi waunda sera ya lugha hata baada ya ukoloni.

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, ilibainika kwamba mielekeo hasi ilijitokeza kutoka kwa watafitiwa waliokiona Kiswahili kama lugha isiyo na manufaa ya kiuchumi katika soko la kimataifa. Kwa maoni ya watafitiwa, Wakenya wengi, hata wadau katika mchakato wa utekelezaji wa sera ya lugha, wamerithi mielekeo ya jadi ambapo lugha ya Kiingereza ilihusishwa na elimu nzuri iliyomwezesha mwanajamii kufanikiwa kupata ajira nzuri hivyo, kupanda ngazi kijamii na kiuchumi. Mtazamo huu umeegemewa na watafitiwa walio katika kundi lenye umri wa miaka 31 na zaidi, ila wale wa jinsia ya kike ndio wanaushikilia kwa nguvu zaidi. Utafiti huu unadadisi ikiwa wadau hawa watabadili mielekeo yao kuhusu majukumu ya lugha ya Kiswahili katika kipindi ambapo Kiswahili kimekwezwa kihadhi na katiba ya Kenya.

Kutokana na mahojiano na watafitiwa, ilibainika kwamba wengi wao bado hawajafahamu kwamba Kiswahili kimepewa hadhi ya kuwa lugha rasmi nchini Kenya. Hii inamaanisha kwamba ingawa Katiba ya Kenya imekitambua Kiswahili kwa kukikweza kihadhi, wadau katika uundaji sera na katika mchakato wa utekelezaji wa sera ya lugha kama vile walimu wana wajibu wa kuwahamasisha wadau wa mashinani kuhusu kauli kama hizi za kikatiba zinazorejelea suala muhimu kama hili la lugha.

4.2 Masiala Yanayosababisha Mielekeo Kuhusu Kiingereza

Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu, lugha ya Kiingereza ndiyo inayopendelewa na watafitiwa wengi kama lugha rasmi nchini Kenya. Waliodhihirisha mielekeo chanya kuhusu jukumu rasmi la Kiingereza walishawishiwa na hali kwamba Kiingereza ni lugha ya kimataifa. Kwa hivyo, kupitia matumizi rasmi ya lugha hii, mtu ataweza kuimudu na kukwea kijamii na kiuchumi, kwa kuhusika kimataifa kama vile katika ulimwengu wa biashara, teknolojia na elimu.

Ingawa sio watafitiwa wengi waliopendelea matumizi rasmi ya Kiingereza kwa sababu jumishi, wachache wa watafitiwa hawa walikihusisha Kiingereza na tabaka la kifahari kwa kuchukulia kwamba wanaokitumia Kiingereza hudhihirisha upeo wa juu katika elimu. Kwao, kuzungumza kwa lugha hii ya Kiingereza hudhihirisha utambulisho aula wa kijamii, kwamba mhusika ni mmojawapo wa wale walio katika tabaka la juu katika jamii.

Masiala ya kihistoria pia yamesababisha watafitiwa kuwa na mielekeo chanya kuhusu jukumu rasmi la lugha ya Kiingereza. Kutoka enzi ya kikoloni nchini Kenya watafitiwa walihoji kuwa lugha ya Kiingereza imetambuliwa kama lugha bora ya kutumika katika miktadha rasmi. Kwa watafitiwa hawa, huu ni mtazamo ambao ulirithiwa na Wakenya wengi hata baada ya Kenya kujipatia uhuru. Kiingereza ndiyo lugha iliyotumika kirasmi (kufundishia) katika mfumo wa elimu hadi Kiswahili kilipokwezwa hadhi katika Katiba ya mwaka wa 2010. Kwa hali hii, mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiingereza haijabadilika

Watafitiwa walipoulizwa kutoa maoni yao kuhusu uwezekano wa kusawazisha matumizi ya lugha ya Kiingereza na ile ya Kiswahili kama lugha mbili rasmi, wengi walikubali. Waliokubali walieleza kuwa hili linawezekana hasa shuleni ambapo usambamba huu unaweza kubuniwa taratibu za kufuatwa ili kuepuka matumizi mapotovu ya lugha zote mbili kwa madai ya kuzisawazisha. Taratibu zilizopendekezwa ni kama vile kutenga idadi sawa ya siku za wiki

ambapo lugha hizi zitatumiwa. Usawazishaji huu utaziwezesha lugha zote mbili kukua na kutambulika kihadhi. Pendekezo hili linaendana na kauli ya Katiba ya Kenya ya utunzaji, ukuzaji na uendelezaji wa matumizi ya lugha tofautitofauti za Wakenya. Vinginevyo, hali ya uwililugha rasmi kama ilivyo Canada huweza kudumishwa.

Watafitiwa waliopinga uwezekano wa kusawazisha matumizi ya lugha zote mbili walilalamikia uhaba wa vifaa vya kujifunzia kwa usambamba kwani masomo mengine yote hufundishwa kwa lugha ya Kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili. Wengine wasiopendelea matumizi rasmi ya Kiingereza na Kiswahili walidai kuwa Kiswahili hakijakomaa kimsamiati. Utafiti huu uligundua kuwa madai haya yanatokana na sababu za kihistoria. Wengi wa watafitiwa waliopinga kauli hii hawakufundishwa lugha ya Kiswahili katika mfumo wa zamani wa elimu. Kwa hiyo, masiala ya kihistoria kuhusu lugha katika mfumo wa elimu vilevile yana nafasi katika mielekeo kuhusu matumizi ya lugha ya Kiingereza na Kiswahili kama lugha mbili rasmi nchini Kenya.

Watafitiwa wachache waliodhihirisha mielekeo hasi kuhusu ukuzaji wa lugha ya Kiingereza waliafikiana na madai ya wanaharakati wa lugha kama vile Ngugi wa Thiong'o kwamba kukuza lugha ya mkoloni ni kuendeleza ukoloni wa kilugha na utamaduni wa mkoloni (wa Thiong'o 1986). Hapa, masiala ya kihistoria yana nafasi kubwa katika mielekeo hasi kuhusu ukuzaji wa Kiingereza kama mojawapo ya lugha za Wakenya.

4.3 Masiala Yanayosababisha Mielekeo Kuhusu Lugha Asilia (Kimeru)

Katika mahojiano kuhusu lugha iliyopendelewa kutumiwa katika kujazia hojaji, watafitiwa wote walidhihirisha mielekeo iliyopinga matumizi ya lugha ya Kimeru kujazia hojaji. Mielekeo yao ilisababishwa na masiala ya kiisimu ambapo walihofia upeo wa chini katika uwezo wao wa kujieleza kimaandishi kwa kutumia lugha hii ya Kimeru. Hata hivyo, mtafiti alipowatazama watafitiwa walipotangamana na wenzao majilisini, wengi walipendelea mazungumzo kwa lugha

ya Kimeru. Vilevile walionekana, mara nyingi, wakiwasiliana na wanafunzi ama kwa lugha asilia ya Kimeru au kwa kuchanganya lugha hii na ile ya Kiswahili.

Mielekeo chanya ya walimu kuhusu matumizi ya Kimeru iliongozwa na masiala ya kijamii. Wengi wa watafitiwa walipendelea kutumia lugha yao asilia kama kitambulisho cha kijamii. Kupitia utambulisho wa aina hii wengi wa watafitiwa walieleza kwamba kupitia matumizi ya lugha asilia ya Kimeru, utamaduni hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Aidha Lugha asilia ilielezwa kama nyenzo ya kurahisisha mawasiliano ya kinyumbani hivyo hukuza utangamano miongoni mwa wanajamii-lugha.

Isitoshe, matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kwamba mwito wa Wizara ya Elimu nchini Kenya, kuhusu kufundishia kwa kutumia lugha asilia katika madarasa ya mwanzomwanzo hadi darasa la tatu ni juhudi ya kukuza lugha mbalimbali za Wakenya. Sababu kuu iliyotolewa kuhusu kauli hii ya wizara ni kwamba lugha asilia ni nyenzo ya kurahisisha mawasiliano baina ya walimu na wanafunzi wao ili kuyamudu wanayofundishwa. Vilevile upendeleo wa matumizi ya lugha asilia katika kufundishia ulielezwa kuwa mojawapo ya njia za kukuza na kuendeleza utamaduni wa jamiilugha husika. Wengine miongoni mwa watafitiwa hawa walilalamika kwamba lugha asilia hazijapewa nafasi ya kukua kutokana na madai kwamba lugha hizi hazifundishwi tena baada ya darasa la tatu. Watafitiwa walipendelea mfumo wa elimu unaoruhusu ufundishaji kwa lugha hizi asilia katika shule za msingi nchini Kenya.

Watafitiwa waliodhihirisha mielekeo hasi kuhusu ukuzaji na uendelezaji wa lugha asilia Kenya walitoa maoni kwamba kufanya hivyo ni kutukuza ukabila nchini. Hawa waliongozwa vilevile na mtazamo kwamba lugha asilia hazina manufaa ya kujiinua kijamii na kiuchumi. Sababu ya watafitiwa hawa kuwa na mwelekeo kama huu ni kwamba nchini Kenya mfumo wa elimu hutilia mkazo zaidi upitaji wa mitihani ya kitaifa. Hili husasababisha walimu, wanafunzi na wazazi

kusisitiza matumizi ya lugha ya Kiingereza na Kiswahili hata katika muktadha wa kinyumbani. Kwa hivyo umuhimu wa lugha asilia Kenya unadidimia huku ule wa lugha tahiniwa ukiimarika.

4.4 Masiala Yanayosababisha Mielekeo Kuhusu Lugha Ishara ya Kenya na Breli

Watafitiwa walidhihirisha mielekeo chanya kuhusu kauli ya Katiba kwamba serikali italinda na kuendeleza matumizi ya Lugha Ishara ya Kenya na Breli, pamoja na miundo mingine inayoweza kufikiwa na watu wenye changamoto za kimaumbile. Mielekeo yao iliongozwa na suala la haki za matumizi ya lugha, ambapo walieleza kwamba walemavu pia wana haki ya kuelezwa na kujieleza kwa lugha wanayoifahamu. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu masiala ya kijamiinafia kwa upande wa walemavu pia yalitawala ambapo, kwa maoni ya walimu waliotafitiwa, walemavu wanafaa kutambuliwa na kujitambulisha kama wanajamii wenye haki ya kujumuika na wengine katika ujenzi wa taifa la Kenya. Walimu watafitiwa katika eneo hili walikubali kauli hii kama wito wa serikali wa kuwatambua wanajamii hawa kama kiungo kimoja cha Wakenya, jambo ambalo limekuwa likitekelezwa katika mfumo wa elimu pekee. Baadhi ya wqatafitiwa waliungama kuwa wanao jamaa walio na aina hizi za ulemavu na kwa hiyo, wanahitaji watumizi ya Lugha Ishara pamoja na Breli. Matumizi ya misimbo hii ya mawasiliano huweza kupunguza unyanyapaa unaokwenda na aina hizi za ulemavu.

4.5 Hitimisho

Kutokana na matokeo ya utafiti wetu, tumeyajadili masiala yanayosababisha mielekeo ya watafitiwa kuhusu suala la lugha lililojitokeza katika Katiba ya Kenya ya 2010. Masiala haya yanaangazia lugha ya Kiswahili, Kiingereza, lugha asilia ya Kimeru, Lugha Ishara ya Kenya na Breli. Masiala yanayotawala mielekeo ya watafitiwa yalikuwa ya kihistoria, kijamii, kiisimu na kiuchumi.

Mielekeo chanya kuhusu Kiswahili kama lugha ya taifa na rasmi nchini Kenya imeongozwa na masiala ya kijamii ya ujitambulishaji wa Wakenya kama jamii moja. Sababu za kiuchumi ziliwasababisha watafitiwa wengine kuwa na mielekeo hasi kuhusu Kiswahili kwa madai kwamba hakihusishwi na hadhi ya juu inayomwezesha mtu kupata ajira nzuri, kinyume na Kiingereza kilichochukuliwa kama lugha ya kimataifa, inayompa mtu fursa ya kupata kazi bora.

Upendeleo wa matumizi ya lugha asilia vilevile uliongozwa na masiala ya kijamii ya kutaka kujihusisha na kuwasiliana miongoni mwa wanajamiilugha moja ya Kimeru. Hii ilidhihirika hata kwa utazamji wa watafitiwa waliotekeleza mawasiliano kwa lugha yao asilia ya Kimeru.

Sababu za kimawasiliano na kisaikojamii ziliongoza mielekeo ya watafitiwa kuhusu ukuzaji wa Lugha Ishara ya Kenya na Breli kwa walemavu wapatikanao nchini Kenya.

Katika sura ifuatayo, tunaangazia muhtasari wa utafiti huu, hitimisho na mapendekezo kwa watafiti wa baadaye mbali na kuangazia changamoto tulizokumbana nazo katika utafiti wetu.

SURA YA TANO

MUHTASARI, CHANGAMOTO ZA UTAFITI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.0 Utangulizi

Utafiti huu ulikuwa ukichunguza mielekeo ya walimu wa shule za msingi kama kundi mojawapo la wadau wa kimsingi katika mchakato wa utekelezaji wa sera ya lugha nchini Kenya kama inavyoelezwa katika Katiba ya Kenya ya mwaka wa 2010. Uchunguzi kuhusu mielekeo ya wadau hawa iliangazia kauli zinazohusu suala la lugha kama linavyojitokeza katika Ibara ya 7 sehemu ya 1, 2 na 3 ya Katiba hii. Kauli hizi ni zifuatazo:

- (1) Lugha ya taifa ni Kiswahili
- (2) Lugha rasmi za taifa la Kenya ni Kiswahili na Kiingereza
- (3) Serikali:
 - (a) itakuza na kutunza lugha tofautitofauti za Wakenya
 - (b) Serikali itakuza na kuendeleza matumizi ya lugha za kienyeji, Lugha Ishara ya Kenya, Breli na miundo mingine ya kimawasiliano inayoweza kufikiwa na walemavu (Katiba ya Jamhuri ya Kenya 2010).

Katika kuangazia kauli hizo za Katiba ya Kenya zinazoshughulikia suala la lugha nchini Kenya, tulitumia nadharia ya Kijamii ya Fishman (1968) na vilevile nadharia ya Kijamiinafsia ya Lambert (1963). Nadharia ya Kijamii inaeleza kuwa tabia ya wanajamii kuhusu lugha huhusisha matumizi na vilevile mielekeo ya watumizi kuhusu lugha husika, suala linalotegemea muktadha wake wa matumizi. Nadharia ya Kijamiinafsia nayo inaeleza kuwa maoni ya wanajamii kuhusu

lugha fulani kuambatana na majukumu yanayohusishwa na lugha fulani hudhihirisha mielekeo yao kuhusu lugha husika na kuhusu watumizi wake.

Utafiti huu ulilenga kuchunguza mielekeo ya walimu wa shule za msingi kama washikadau wa kimsingi katika utekelezaji wa suala la lugha kama linavyoelezwa katika Katiba ya Kenya.

Katika utafiti wetu tulilenga kujibu maswali yafuatayo:-

- i. Je, walimu wa shule za msingi Wilayani Igembe Kaskazini wana mielekeo gani kuhusu matumizi ya Kiswahili kama Lugha ya Taifa nchini Kenya?
- ii. Je, walimu wa shule za msingi Wilayani Igembe Kaskazini wana mielekeo gani kuhusu jukumu la Kiswahili kama lugha rasmi nchini Kenya?
- iii. Je, walimu wa shule za msingi Wilayani Igembe Kaskazini wana mielekeo gani kuhusu matumizi ya Kiswahili na Kiingereza kama lugha mbili rasmi shuleni?
- iv. Je, ni ipi mielekeo ya walimu wa shule za msingi Wilayani Igembe Kaskazini kuhusu kauli ya Katiba kwamba serikali itakuza na kuendeleza matumizi ya lugha asilia za Wakenya?
- v. Je, ni ipi mielekeo ya walimu wa shule za msingi Wilayani Igembe Kaskazini kuhusu kauli ya Katiba kwamba serikali itakuza na kuendeleza matumizi ya Lugha Ishara ya Kenya na Breli na njia nyingine za mawasiliano na teknolojia zinazoweza kufikiwa na watu wenye ulemavu?

Ili kutimiza madhumuni ya utafiti huu, tulitafuta data ya kimsingi kutoka kwa walimu wa shule za msingi katika wilaya ya Igembe Kaskazini, kama wadau wa mashinani katika mchakato wa utekelezaji wa kauli za katiba zinazoangazia suala la lugha nchini Kenya. Data ilikusanywa kwa njia ya hojaji, mahojiano yasiyokuwa ya moja kwa moja na vilevile utazamaji wa tabia za matumizi ya lugha kutoka kwa watafitiwa. Tuligawa kazi yetu katika sura tano.

Katika sehemu inayofuata tunatoa muhtasari wa kila sura.

5.1 Muhtasari

Kwa jumla, sura ya kwanza ni utangulizi wa kazi hii.

Katika sura ya pili, tumeangazia historia ya mielekeo ya Wakenya kuhusu lugha nchini Kenya.

Katika sura hii, tumejadili mielekeo kuhusu lugha katika enzi ya ukoloni na kueleza jinsi mielekeo hiyo ilivyoathiri mielekeo waliyokuwa nayo watu wa Kenya kuhusu lugha hata baada ya kujiokoa kutoka kwa wakoloni. Aidha katika sura hii ya pili, tumejadili suala la lugha katika katiba za awali na katiba ya sasa nchini Kenya kwa madhumuni ya kutofautisha jinsi suala hili la lugha lilivyoshughulikiwa na kila moja. Kwa kuwa utafiti wetu unahusisha Katiba ya sasa ya Kenya, pia tumejadili sera ya lugha kwa mujibu wa Katiba hii.

Matokeo ya utafiti huu yamewasilishwa katika sura ya tatu. Mielekeo ya watafitiwa kuhusu majukumu na matumizi ya lugha ya Kiswahili, Kiingereza, Kimeru (kama lugha asilia), Lugha Ishara ya Kenya na Breli imejadiliwa kwa kuangazia matokeo ya utafiti huu. Imebainika kuwa ipo mielekeo chanya na vilevile hasi kutegemea majukumu ya lugha husika. Kauli ya Katiba ya Kenya kuhusu ukuzaji na uimarishaji wa Lugha Ishara ya Kenya na Breli ndiyo misimbo pekee iliyojitokeza kuvutia mielekeo chanya pekee. Hakukuwa na mtafitiwa yeyote aliyedhihirisha mwelekeo hasi kuhusiana na kauli ya Katiba iliyoeleza kuhusu misimbo hii ya Lugha Ishara na Breli.

Sura ya nne imeshughulikia masiala yaliyosababisha mielekeo ya watafitiwa kuhusu majukumu na matumizi ya lugha mbalimbali zizotajwa hapo juu, kama yalivyojitokeza katika utafiti huu. Kutokana na utafiti huu, masiala yaliyojitokeza kuwa kiathiri cha mielekeo ya watafitiwa ni yale ya kihistoria, kijamii, kiisimu na kiuchumi. Masiala hayo yalisababisha mielekeo chanya au hasi kuhusu lugha husika kama zilivyoelezewa katika kauli za Katiba ya Kenya ya mwaka wa 2010.

5.2 Changamoto za Utafiti

Utafiti ulikumbwa na changamoto kadha wa kadha. Hata hivyo mtafiti alijitahidi na kuukamilisha. Changamoto kuu ilikuwa muda mrefu uliotumika katika kukusanya data. Ukusanyaji wa data ulinuiwa kuchukua muda wa wiki mbili, ambapo mtafiti angekusanya data kutoka kwa walimu wa kila eneo la utafiti kwa muda wa siku mbili. Hili halikutimika kama lilivyopangwa. Badala yake, ilimchukua mtafiti muda katika kuwafafanulia watafitiwa kuhusu suala la lugha lilivyoelezwa katika Katiba ya Kenya. Hii ni kwa sababu wengi wa watafitiwa hawakuwa na ufahamu wa awali kuhusu katiba inavyoeleza kuhusu suala la lugha nchini Kenya. Ukusanyaji wa data hivyo basi ulikamilika baada ya wiki nne badala ya wiki mbili zilizopangwa. Vilevile, ilimhitaji mtafiti kuwa na uvumilivu kwa maelezo ya kina ili baadhi ya watafitiwa wakubali kujaza hojaji za utafiti. Hata hivyo, hili lilitokea tu kwa baadhi ya walimu hasa wale wa shule za vijijini zilizo mbali zaidi na miji wala sio shule zote katika wilaya iliyofanyiwa utafiti huu.

5.3 Mahitimisho

Kwa kuhitimisha, utafiti huu umedhihirisha kwamba kwa jumla, walimu wa shule za msingi wana mielekeo chanya kuhusu suala la lugha kama linavyojitokeza katika Katiba ya Kenya iliyoidhinishwa mwaka wa 2010. Walimu hao walidhihirisha mielekeo chanya kuhusu dhima ya Kiswahili ya kutumika kama lugha rasmi nchini Kenya. Wengi wa watafitiwa waliohojiwa waliafikiana na kauli kwamba kutumia Kiswahili kama lugha rasmi katika miktadha rasmi ni mojawapo ya mbinu za kuikuza na kuistawisha lugha hii ili iweze kutekeleza jukumu lake kama lugha inayowatumikia Wakenya.

Vilevile, watafitiwa hawa walikuwa na maoni yaliyokubali jukumu la Kiswahili kama lugha ya taifa la Kenya. Hata hivyo, walimu waliohojiwa walikariri kwamba ingawa imepangwa kihadhi kwa kupewa majukumu mbalimbali nchini Kenya, lugha ya Kiswahili inahitaji kushughulikiwa zaidi kwa kuundiwa msamiati zaidi kutegemea uhitaji na kuandikiwa vitabu mbalimbali. Kwa kupangwa hivi lugha hii itajitosheleza na kukubalika na Wakenya walio wengi kama lugha inayowatambulisha kama jamiilugha moja yenye utamaduni sawa.

Kauli ya Katiba kuhusu matumizi ya lugha ya Kiingereza kama lugha rasmi sambamba na ile ya Kiswahili ni kauli inayoafikiwa na watafitiwa walio wengi. Hata hivyo, utafiti huu ulipata kugundua kwamba masiala ya kihistoria kuhusu hadhi za lugha hizi mbili yaliathiri mielekeo ya walimu kuzihusu. Masiala haya yalijitokeza, kwa mfano, pale ambapo baadhi ya wahojiwa walikipendelea Kiingereza kwa kudai kuwa wao walipitia mfumo wa zamani wa elimu ambapo Kiingereza kilienziwa kuliko Kiswahili kwa kufundishwa na kutahiniwa katika ngazi za shule ya msingi, sekondari na vyo vya ualimu.

Mielekeo ya walimu waliohojiwa kuhusu kauli ya katiba inayoegemea ukuzaji na uendelezaji wa lugha asilia ilidhihirika kuwa chanya. Watafitiwa walio wengi waliunga mkono kauli hii kwa kuongozwa na nia ya kuzitumia lugha hizi katika, kwanza, kufanikisha mawasiliano katika miktadha husika na, pili, kujitambulisha kama wanajamii wa jamiilugha moja yenye tamaduni tofauti na zile nyingine. Hili lilidhihirika pale wengi wa waliohojiwa walipendelea kutumia lugha ya Kimeru mara nyingi walipowasiliana wao kwa wao majilisini na walipowasiliana na wanafunzi nje ya madarasa. Hata hivyo, ilibainika kuwa juhudi za wadau wote katika upangaji lugha zilihitajika ili kuwepo vitabu zaidi vilivyochapishwa kwa lugha asilia ili kuweza kufundishia lugha hizi.

Walimu wote waliohojiwa walidhihirisha mielekeo chanya kuhusu kauli ya katiba inayoegemea ukuzaji na uendelezaji wa Lugha Ishara ya Kenya na vilevile Breli. Wahojiwa walikiri kwamba walemavu ama wasiosikia au wasioona ni watu wanaohitaji kutambuliwa kama wanajamii muhimu nchini Kenya ili kupunguza unyanyapaa unaokwenda na hali husika za ulemavu. Isitoshe, watafitiwa walieleza kuwa kwa kutumia Lugha Ishara ya Kenya na Breli walemavu hawa watapata fursa ya kuwasiliana na Wakenya wengine na kwa hiyo, watapata fursa ya kuhusishwa katika shughuli za uendelezaji wa taifa.

5.4 Mapendekezo

Kutokana na matokeo ya utafiti wetu, tumetambua kwamba ingawa walimu wa shule za msingi wanadhihirisha mielekeo chanya inayouona umuhimu wa kutekeleza kauli za Katiba ya Kenya zinazohusiana na suala la lugha, utekelezaji huu wa suala la lugha katika Katiba haujafaulu hasa katika mfumo wa elimu. Wadau hawa wamelalamika kuwa wao wanafaa kupigwa jeki na wadau kama vile serikali na wapangaji lugha wengine ili kufaulisha mchakato huu. Hivyo basi tunapendekeza serikali ibuni mikakati ya kuiwezesha kufadhili mfumo wa kuwaandaa walimu kwa ufanikishaji wa utekelezaji wa kauli za Katiba zinazohusu suala la lugha nchini Kenya. Hili litawaepusha walimu kuwa katika hali ya kilinge inayokwenda na kuhubiri maji ilhali wao wanywa mvinyo kama wadau wa kimsingi katika utekelezaji wa sera ya lugha nchini Kenya.

Kutokana na utafiti huu, tunapendekeza kwamba wadau katika masuala ya lugha nchini Kenya wanafaa pia kubuni mikakati ya kuwawezesha walimu kama wale waliotafitiwa kufanikisha matumizi rasmi ya Kiswahili na Kiingereza bila upendeleo wa lugha moja. Hili linaweza kufanywa kwa kuwaandalia wadau hawa mafunzo ya ziada yanayoshughulikia lugha kama ya Kiswahili ambayo wengi wao hawakupata fursa ya kufunzwa katika mfumo wa awali wa elimu. Kwa kufanya hivi wanaohusika watajipusha na hali ya kuhifadhi kauli zinazohusiana na lugha

nchini Kenya kama za kisheria tu katika hifadhi za rekodi, kama ilivyokuwa awali Kiswahili kilipotangazwa kuwa lugha rasmi.

Isitoshe, twapendekeza pia uandishi na uchapishaji wa vitabu zaidi hasa kwa lugha ya Kiswahili na zile nyingine asilia ili kusambaza maarifa kwa kuzitumia lugha hizi. Hili litaziwezesha lugha hizi kukua na kuimarika kama vyombo vya mawasiliano yanayohusu mada mbalimbali katika nyanja tofautitofauti kama vile katika elimu, sayansi na teknolojia miongoni mwa nyanja nyingine.

Utafiti wetu ulipata kugundua kuwa watafitiwa wanapendekeza hali ambapo kila Mkenya, awe au asiwe mlemavu, anapata fursa ya kujifunza Lugha Ishara ya Kenya na vilevile Breli. Kwa kufanya hivi, kila Mkenya atakuwa ametambuliwa kihaki na kuhusishwa na wengine katika ujenzi wa taifa la Kenya.

Kutokana na uhaba wa fedha na wakati, utafiti wetu ulibanwa katika uchunguzi wa mielekeo ya walimu wa shule za msingi kutoka eneo la mashambani ambapo takriban wote wana lugha moja asilia. Walimu sio wadau wa pekee katika utekelezaji wa kimsingi wa sera ya lugha nchini Kenya. Mielekeo ya wadau wengine wa kimsingi katika suala hili la lugha yaweza kuhusishwa. Mielekeo kuhusu sera ya lugha hutegemea pia mazingira wanamojipata wadau husika na lugha walizozoea kutumia. Kwa sababu hizi tunapendekeza tafiti zaidi kufanywa kuhusu masuala yafuatayo:

(i) Utafiti unaohusisha walimu katika shule za msingi mijini ili kupima mielekeo yao kuhusu

suala la lugha katika Katiba ya Kenya.

(ii) Utafiti ufanywe kwa kuhusisha wadau wengine kama vile wazazi na wahubiri ili

kuchunguza mielekeo yao kuhusu majukumu mbalimbali yaliyopewa lugha katika Katiba

ya Kenya.

(iii) Mielekeo ya wanafunzi wa vyo vikiu inaweza kuchunguzwa ili kupima ukubalifu wao kuhusu majukumu yanayohusishwa na lugha mbalimbali katika Katiba ya Kenya.

MAREJELEO

Abdulaziz, M. H. (1982) Patterns of of Language Acquisition and Use in Kenya: Rural - Urban

Differences. Katika Polome, E. (Mhr). *International Journal of the Sociology of Language*. Vol.34.

Adoyo, P. O. (2002) *Emergent Approaches Towards Sign Bilingualism in Deaf Education in*

Kenya. Stichproben: Wiener Zeitschrift Fur Kristische Afrikanstuden.

Agheyisi, R. na Fishman, J.A. (1970) Linguistic Attitude Studies: A Brief Survey of

Methodological Approaches. *Anthropological Linguistics*. 12 (5), 131-157.

Allport, G.W. (1954) Attudes in the History of Social Psychology. Katika Warren, Neil, Jahoda

na Marie (1966). *Attitudes in the History of Social Psychology*.

Harmondsworth: Penguin Books.

Baker, C. (1992) *Attitudes to Language*. Clevedon: Multilingual Matters.

Cargile, A.C., Giles, H. (1997) Understanding Language Attitudes: Exploring Affect and

Identity. *Language and Communication*. 17 (3), 195-217.

Chimera, R. (1998) *Kiswahili Past, Present and Future Horizons*. Nairobi: Nairobi University

Press.

Chiraghdin, S. na Mnyampala, M. (1977) *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University

Press.

Greenberg, J. H. (1963) Languages of Africa. Nyongeza katika *International Journal of American Linguistics*, 29.1.

Fink, T. K. (2005) *Attitudes Towards Languages in Nairobi*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Pittsburgh.

Fishman, J. A. (1972) *Sociolinguistics*. Massachusetts: Newbury House Publishers.

Gardner, R.C. na Lambert, W.E. (1972) *Attitudes and Motivation in aSecond-Language Learning*. Massachusetts: Newbury House Publishers.

Giglioli, P. (1972) *Language and Social Context*. Middlesex: Penguin Books.

Githinji, P. (2008) Ambivalent Attitudes: Perception of Sheng' and its Speakers. Ohio University: *Nordic Journal of African Studies*. 17(2), 113-136.

Gorman, T.B. (1974) The Development of Language Policy in Kenya with Particular Reference to the Educational System. Katika. Whiteley, W.H. (mhr). *Language in Kenya*. Nairobi: Oxford University Press. 397-446.

Ihemere, K. U. (2006) An Integrated Approach to the Study of Language Attitudes and Change in Nigeria: The Case Study of the Ikwerre of Port Harcourt. Katika Olaba, F. A. na Michael, A.P. (whr), *African Linguistics* (pp. 194-207). Somerville, MA: Cascadilla.

Jones, J. M. (2012) The Effect of Language Attitudes on Kenyan Stakeholder Involvement in

Mothertongue Policy Implementation. *Journal of Multilingual and Multicultural Development*. 33(3), 237-250.

Kembo - Sure (2002) Language Planning and National Development in Kenya. Katika: Ingrid R. (mhr). *Languages in Contact*. Bayreuth: African Studies. Vol.51.

Kibiwott, P. K. (2006) *The Future of Languages of Kenya: Adopting the Principles of Environmental Conservation*. Makala yaliyowasilishwa katika Kongamano la BAAL Linguistics in Africa Special Interest Group, Chuo Kikuu cha London.

King'ei, K. (2010) *Misingi ya Isimujamii*. Dar es Salaam: TUKI.

Kobia, J.M. na Ndiga, T.K. (2013) The Influence of Secondary School Students' Attitudes Toward the Implementation of Kiswahili Curriculum in Igembe South District, Meru County, Kenya. *International Journal of Education and Research*. 12(1), 1-12.

Lambert, W.E. (1963b) Approaches to the Study of Language Part II: On the Second Language Learning and Bilingualism. *The Modern Language Journal*. 47(14), 114-121.

Lambert, W.E., Hodson, R., Gardner, R.C. na Fillenbaum, S. (1960) Evaluational Reactions to Spoken Languages. *Journal of Abnormal and Social Psychology*. 60(1), 44-51.

Mathooko, P.M. (2007) *Isimujamii: Misingi na Nadharia*. Nairobi: Njigua Books.

Mazrui, A. M. (1978) The Religious Factor in Language Nationalism: The Case of Kiswahili in

Kenya. Katika: *Studies in African Linguistics*. Vol.9. No. 21978. University of California.

Mbaabu, I. (1991) *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*. Nairobi: Longman Kenya.

_____ (1996) *Language Policy in East Africa*. Nairobi: Educational Research Publications.

McKeown, C. (2008 ed.) *Collins Concise English Dictionary*. Glasgow: HarperCollins Publishers.

Mohochi, S. (2011) Mielekeo ya Wasomi wa Kiswahili na Viongozi wa Afrika Mashariki Kuhusu Lugha ya Kiswahili. *Swahili Forum*. 18: 24-36.

Mukhwana, A. (2008) *Language Attitudes in Urban Kenya: The Case Study of Kisumu, Nairobi and Mombasa*.Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijchapishwa, Chuo Kikuu cha Nairobi.

_____ (2013) A New Language Policy but Old Language Practices: The Case of Kenya After 2010 Constitution. *International Journal of Innovative Research and Development*. Vol.2 No. 9.

Mukhwana, A. na Jerono, P. (2014) Language Attitudes in Colonial Kenya: An Historical Perspective. *International Journal of Education and Research*. Vol.2 No.3.

Ngidi, S.A. (2007) *The Attitudes of Learners, Educators and Parents Toward English as a*

Language of Learning and Teaching in Mthunzini Circuit. Tasnifu ya Uzamili

ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Zululand.

Njoroge, J. (1990) Multilingualism and Some of its Implications for Language Policy and

Practices. Katika Legere, K. (mhr). *The Role of Language in Literacy*

Programmes with Special Reference to Kiswahili. Bonn: German Foundation for

International Development. (249- 269).

Ogola, J.O. (1990) *Mielekeo ya Wasomi kuhusu Matumizi ya Lugha ya Kiswahili Nchini Kenya*.

Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Republic of Kenya (1964) *Kenya Education Report Part I(Ominde Report)*. Nairobi:

Government Printer.

_____ (1976) *Kenya Education Commission Report Part (Gachathi Report)*.

Nairobi: Government Printer.

_____ (1984) *Second University in Kenya: Report of Presidential Working Party*

(Macky Report). Nairobi: Government Printer.

_____ (2010) *The Constitution of the Republic of Kenya, 2010*. Nairobi: National

Council for Law Reporting.

Romaine, S. (1980) Stylistic Variation and Evaluative Reactions to Speech: Problems in the

Investigation of Linguistic Attitudes in Scotland. *Language and Speech*. 23:213-

Schiffman, H. (1996) *Linguistic Culture and Language Policy*. London: Routledge.

Smith, M.K. (1996) Curriculum Theory and Practice. *The Encyclopaedia of Informal Education*.

www.infed.org/biblio/b-curric.htm.

TATAKI (2013) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: TUKI.


wa Thiong'o, N. (1986) *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Literature*.

Nairobi: East African Educational Publishers.

Whiteley, W. H. (1974) *Language in Kenya*. Nairobi: Oxford University Press.

KIAMBATISHO A

BARUA YA UTAMBULISHO



UNIVERSITY OF NAIROBI

Department of Kiswahili

Telegrams: "Varsity" Nairobi

P. O. Box 30197

Telephone: Nairobi 318262 Ext 28063

NAIROBI, KENYA.

27/5/2014

TO WHOM IT MAY CONCERN

ROSE KAUMEURU MIRIANGA – C50/79831/2012

The above named is a student registered in the Department of Kiswahili at the University of Nairobi for her postgraduate programme. She intends to conduct her M.A. research in Igembe North Primary Schools.

Any assistance accorded to her will be highly appreciated because it will assist her finalize her research and project.

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'John Habwe'.

Prof. John Habwe
Chairman, Department of Kiswahili

KIAMBATISHO B

HOJAJI YA UTAFITI KWA LUGHA YA KISWAHILI

HOJAJI YA UTAFITI

Mimi ni mwanafunzi wa shahada ya Uzamili katika Idara ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Nairobi. Nimekuja kwako ili kukuomba msaada wako katika kujaza hojaji hii inayohusu masomo yangu.

Mielekeo Kuhusu Suala la Lugha Katika Katiba ya Kenya.

Utafiti huu unakusudia kuchunguza mielekeo ya walimu wa shule za msingi kuhusu suala la lugha kama lilivyoelezwa katika Katiba ya Kenya ya 2010. Inatarajiwa kuwa matokeo ya utafiti huu yatawafaidi wanaohusika katika masuala ya upangaji lugha kupanga mikakati inayofaa ili kudhibiti hali ya lugha nchini Kenya. Maoni yako kama mwanajamii mwenye uelewa zaidi kuhusu suala la matumizi ya lugha shuleni na nchini Kenya kwa jumla yatakuwa mchango muhimu katika utafiti huu. Majibu yako kwa maswali yafuatayo yatatumiwa kwa shughuli ya kiutafiti tu na yatakuwa ya siri. Kwa hivyo, tafadhali usiandike jina lako kwenye hojaji hii.

Tafadhali jibu maswali yafuatayo kadri ya uwezo wako.

Eneo la Shule (Zone)..... (Chagua **a, b, c, d** au **e**).

(a) Antuambui (b) Kathanga (c) Naathu (d) Ndoleli (e) Ntunene

SEHEMU YA A:

(i) Jinsia: Kike..... Kiume.....

(Tia alama ya × kwenye jibu ulilochagua)

(ii) Umri.....

(Chagua moja kati ya **a,b,c** na **d**)

(a) Kati ya miaka **20** na **30** (b) Kati ya miaka **31** na **40**

(c) Kati ya miaka **41** na **50** (d) **Zaidi** ya miaka **50**

(iii)Umefundisha kwa **muda gani?**

SEHEMU YA B:

(i) (a) **Kiswahili** ni lugha iliyopewa jukumu rasmi nchini Kenya. Kwa maoni yako, Kiswahili chaweza kutumika kama **lugha ya kufundishia** masomo mengine katika **shule za msingi**

Kenya? (Sema **ndio** au **la**)

.....

(b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako

.....
.....
.....

(ii) Je, ungependelea kutumia lugha gani unapowahutubia wanafunzi katika **mikutano nje ya darasa?** (Chagua moja kati ya **a, b, c** na **d**)

- (a) Kiswahili (b) Kiingereza (c) Kimeru (d) Kuchanganya lugha zote tatu

(iii) Toa sababu za jibu ulilochagua

.....
.....
.....

(iv) Maoni yako ni yapi kuhusu kauli ya Katiba ya Kenya kwamba **Kiswahili ni lugha ya Taifa nchini Kenya?**

.....

(v) (a) Kwa maoni yako, kuna manufaa ya **Kiswahili** kutumika kama **lugha rasmi** nchini

Kenya? (Sema **Ndio** au **La**)

.....

(b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako

.....
.....

(vi) (a) Kwa maoni yako, kuna manufaa ya **Kiingereza** kutumika kama **lugha rasmi** nchini

Kenya? (Sema **Ndio** au **La**)

.....

(b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako.

.....
.....

(vii) (a) Kwa maoni yako, kuna uwezekano wa kutumia Kiswahili na Kiingereza kwa usambamba kama lugha mbili rasmi nchini Kenya hasa katika shule za msingi? (Sema **ndio** au **la**)

(b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako.

.....
.....

(viii) Unaweza kusemaje kuhusu upeo wako wa matumizi ya lugha zifuatazo?

(Chagua mojawapo ya majibu haya kwa kila lugha: **upeo wa juu, upeo wa kati, upeo wa chini**)

(a) Kiswahili

(b) Kiingereza

(c) Lugha asilia kama vile Kimeru

(ix) (a) Ni lugha gani unayofikiria inampa mwanafunzi fursa nzuri zaidi ya kupata ajira nzuri katika siku zake za usoni?

(b) Kwa nini?

.....

(x) (a) “Ninayaonea fahari mazungumzo rasmi kwa kutumia lugha ya **Kiingereza** kuliko **Kiswahili** au **Kimeru**.” (Sema **ndio** au **la**)

(b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako.

.....

.....

(xi) (a) “Ninayaonea fahari mazungumzo rasmi kwa kutumia lugha ya **Kiswahili** kuliko **Kiingereza.**” (Sema **ndio** au **la**).

.....

(b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako.

.....

.....

(xii) (a) “Ninayaonea fahari mazungumzo ya nyumbani kwa kutumia **lugha yangu asilia** kuliko lugha ya **Kiswahili** au **Kiingereza.**” (Sema **ndio** au **la**).....

(b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako.

.....

.....

(xiii) (a) Baina ya Kiingereza na Kiswahili, ungependelea kutumia lugha ipi kutoa **hotuba rasmi?**

(b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako.

.....

.....

(xiv) (a) “Kuna manufaa katika kutunza, kukuza na kuendeleza matumizi ya **lugha za kienyeji** za Wakenya kama vile lugha ya Kimeru.” (Sema **ndio** au **la**)

.....

(b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako.

.....
.....
.....

(c) Kwa maoni yako, Serikali ya Kenya inaweza kutumia mbinu gani ili kuweza kukuza,

kulinda na kustawisha matumizi ya **lugha za kienyeji** za Wakenya?

.....
.....

(xv) (a) Kauli ya Waziri wa Elimu Jacob Kaimenyi ni kwamba lugha asilia zitumike kama lugha ya

kufundishia kutoka madarasa ya chekechea hadi darasa la tatu katika mfumo wa elimu

nchini Kenya. Kwa maoni yako, hii inaweza kuwa mbinu mojawapo ya kulinda na

kustawisha **lugha asilia** za Wakenya? (Sema **ndio** au **la**)

.....

(b) Eleza sababu za jibu lako.

.....
(xvi) (a) “Ni muhimu kwa Serikali kulinda na kustawisha matumizi ya **Lugha Ishara ya**

Kenya, Breli na njia nyingine za mawasiliano na teknolojia zinazoweza kufikiwa na watu wenye ulemavu.” Sema **ndio** au **la**.

.....
(b) Eleza sababu za jibu lako.

.....
(c) Unafikiria serikali inawezaje kulinda na kustawisha matumizi ya **Lugha Ishara ya**

Kenya na vilevile **Breli** ili kufikiwa na watu wenye changamoto za kimaumbile?

.....
.....
(xvii) (a) Kwa maoni yako, ni akina nani kati ya watu wafuatao wanafaa kufunzwa matumizi ya **Lugha Ishara ya Kenya?** (Pigia mstari kwenye jibu).

Wasiosikia pekee, wanaosikia pekee, wanaosikia na wasiosikia

(b) Eleza sababu za jibu lako.....

.....
(xviii) (a) Kwa maoni yako, ni akina nani kati ya watu wafuatao wanafaa kufunzwa matumizi ya **Breli?** (Pigia mstari kwenye jibu).

Wasioona pekee, wanaoona pekee, wanaoona na wasioona.

(b) Eleza sababu za jibu lako

.....

(xix) (a) Kwa maoni yako, ni lugha gani imekomaa kimsamiati nchini Kenya baina ya **Kiswahili** na **Kiingereza**?

(b) Kwa nini?

Ninashukuru sana kwa muda ulionipa. Mchango wako umekuwa muhimu sana katika utafiti huu.

KIAMBATISHO C

HOJAJI YA UTAFITI KWA LUGHA YA KIINGEREZA

RESEARCH QUESTIONNAIRE

I am an M.A. postgraduate student in the Kiswahili Department at the University of Nairobi. I kindly request for your assistance in filling in this questionnaire that concerns my studies.

Attitudes Towards the Language Issue as Provided in the Kenyan Constitution.

This study aims at assessing attitudes of Primary School teachers towards the issue of language as provided in the Kenyan Constitution of 2010. It is expected that the research findings shall benefit those concerned with the language planning matters in laying down appropriate strategies in order to control the language situation in Kenya. Your opinion as a member of the society with better understanding about language use within schools and Kenya as a whole will be of importance in this study. Your answers to the following questions will be used only for research purposes and will be treated as private and confidential. Therefore, please do not write your name on this questionnaire.

Please answer the following questions to the best of your knowledge.

Location of your school (Zone)..... (Choose either **a, b, c, d or e** below)

(a) Antuambui (b) Kathanga (c) Naathu (d) Ndoleli (e) Ntunene

SECTION A:

(i) Gender: Female..... Male.....

(Mark **x** on your answer)

(ii) Age:

(Choose either **a, b, c** or **d** below)

(a) Between **20** and **30** yrs

(b) Between **31** and **40** yrs

(c) Between **41** and **50** yrs

(d) **Above 50** yrs

(iii) For how long have you been teaching?

SECTION B:

(i) (a) **Kiswahili** language has been given an official role in Kenya. In your opinion, should Kiswahili be used as the **language of instruction** in the Kenyan primary schools?

(Choose **Yes** or **No**)

.....

(b) Please give reasons for your answer.

.....

.....

.....

(ii) Which language would you prefer to use when addressing pupils during meetings outside the classroom? (Choose either **a, b, c** or **d**).

- (a) Kiswahili (b) English (c) Kimeru (d) Mixing the three languages

(iii) Please give reasons for your answer.

.....
.....

(iv) What is your opinion about **Kiswahili** as the **national language** of Kenya as provided in the Kenyan Constitution?

.....
.....

(v) (a) In your opinion is there importance of using **Kiswahili** as an **official language** in Kenya? (Say **yes** or **no**).

.....
.....

(b) Please give reasons for your answer

.....

(vi) (a) In your opinion is there importance of using **English** as an **official language** in Kenya? (Say **yes** or **no**).

.....
.....

(b) Please give reasons for your answer

.....
(vii) (a) In your opinion, is it possible to balance the use of **both Kiswahili** and **English** as the official languages especially in primary schools? (Say **yes** or **no**).

(b) Please give reasons for your answer

.....
(viii) What would you say about your ability to use the following languages? (Choose either **High, Moderate** or **Low**)

(a) Kiswahili.....

(b) English.....

(c) Indigenous language e.g. Kimeru.....

(ix) (a) Which language do you think would contribute to a student getting a good employment in future?

(b) Why?

.....
.....
(x) (a) “I am proud of an **official conversation** when using **English** language rather than when i use **Kiswahili**.” (Choose **yes** or **no**).

(b) Please give reasons for your answer.

.....
.....

(xi) (a) “I am proud of an **official conversation** when using **Kiswahili** language rather than when i use **English**.” (Choose **yes** or **no**).

(b) Please give reasons for your answer.

.....
.....

(xii) (a) “I am proud of a **home conversation** when using my **indigenous language** rather than when i use **English** or **Kiswahili**. (Choose **yes** or **no**).

(b) Please give reasons for your answer.

.....
.....

(xiii) (a) Between **English** and **Kiswahili**, which language would you prefer when giving an official speech?

(b) Please give reasons for your answer.....

(xiv) (a) In your opinion, is there importance in protecting, promoting and developing the

use of the **indigenous languages** of the Kenyan people e.g. **Kimeru**? (Say **yes** or **no**).

.....

(b) Please give reasons for your answer.

.....
.....

(c) In your opinion, what strategies can the Kenyan government use in order to promote, protect and develop the use of the **indigenous languages** of the Kenyan people?

.....
.....

(xv) (a) The statement by the Kenyan Education Minister, Jacob Kaimenyi, is that the first languages used in the catchment areas of Kenyan primary schools should be used as the languages of instruction from pre-primary school to standard 3 in the Kenyan education system. In your opinion, do you think this is a strategy of promoting and developing the **indigenous languages** of the Kenyan people? (Choose **yes** or **no**).

(b) Please give reasons for you answer.

.....
.....

(xvi) (a) “It is important for the Kenyan State to protect the development and use of the **Kenyan Sign Language** and **Braille** and **other communication networks** available to people with disabilities” (Say **yes** or **no**).

(b) Please give reasons for you answer.

.....
.....

(c) In your opinion, in what ways can the Kenyan State protect the development and use of the **Kenyan Sign Language** and **Braille** in order makes them available to people with disabilities?

.....
.....

(xvii) (a) In your opinion, who among the following people should be taught the use the **Kenyan Sign Language**? (Underline your answer).

The deaf only, **The hearing only,** **Both the deaf and the hearing.**

(b) Please give reasons for your answer.

.....
.....

(xviii) a) In your opinion, who among the following people should be taught the use of **Braille**? (Underline your answer).

The blind only, **The sighted only,** **Both the blind and the sighted.**

(b) Please give reasons for your answer.

.....
.....

(xix) (a) In your opinion, which language between **Kiswahili** and **English** has a more developed vocabulary?

(b) Why?

.....

Thank you very much for your valuable time. Your contribution has been very vital and of great importance to this study.

KIAMBATISHO D

HOJAJI YA UTAFITI KWA LUGHA YA KIMERU

BIURIA BIA UCUNKUUNI

Uuni ndi muritwa wa University ya Nairobi kuria nkuthoomera Digrii ya ijiri (Masters) rwang'i rwa kithomo kia Kiswahili. Ndeeja gukuroomba uteethio bwaku kiri ucunkuuni bubu buria bukonia mathoomo jakwa.

Mathugaanio Gukonia Migambo Kuriingana na Katiba ya Kenya

Bubu ni ucunkuuni bwa mawooni ya arimu ba cukuru cia mwambiririo (praimari) gukonia migaambo mwanyamwanya kuriingana na uria migambo iji yaariritue ndene ya Katiba ya Kenya ya mwaka ywa 2010. Ni wirigiuro bwakwa ati yaria yakauma kiri ucunkuuni bubu yagateetheria baria babangaga mantu yakonie migaambo mwanyamwanya nthigurune ya Kenya kubaanga mitaratara ya utumiri bwa migaambo nthigurune yeetu ya Kenya. Yaria ukauga ta umwe wa antu baaria bari na uume nkuruki bukonia utumiri bwa migaambo ndeene ya macukuru na ndeene ya Kenya yagatetheeria muno kiri ucunkuuni bubu. Macookio yaku kiri biuria bibi yagatumirwa kiri mantu ya ucunkuuni aki na yakeethirwa yari ya ciri. Niuntu bwa bubu, itu ukeeja kwandika riitwa riaku aja.

Itu cookia biuria bibi ota uria ukoomba we wengwa.

Gicigo kia cukuru (Zone)..... (Taara **a, b, c, d** kana **e**).

(a) Antuambui (b) Kathanga (c) Naathu (d) Ndoleli (e) Ntunene

GICIGO KIA A:

(i) Muntu muka..... Muntu murume.....

(Ikira **x** kiri icookio riaku)

(ii) Ukuru..... (Taara **a, b, c** kana **d**)

(a) Miaka **20 – 30** (b) Miaka **31 – 40** (c) Miaka 41 – 50 (d) **Nkuruki** ya miaka **50**

(iii) Uritaniite igiita ring'ana atia?

GICIGO KIA B:

(i) (a) **Kiswahili** ni mugambo ywei ngugi ya **gutumika kiubici** nthigurune ya Kenya. Kiri wooni bwaku, **Kiswahili** ni kibateerie gutumika ta **mugambo ywa gutumirwa kuritana mathomo yangi** cukuru cia mwambirio (praimari) cia Kenya? (Uga **ii** kana **ari**)

(b) Andika itumi bia icookio riaku

(ii) (a) Ni mugambo juriku ukienda gutumira riria ukwariria aritwa **oome ya kirasi**? (Taara **a, b, c** kana **d**)

.....

(a) Kiswahili (b) Gicunku (c) Kimeru (d) Kuungania migambo jonthe ithatu

(iii) Andika itumi bia icookio riaku

.....

(iv) Wooni bwaku ni buriku gukonia uuge bwa **Katiba ya Kenya** ati **Kiswahili** ni **mugambo ywa nthiguru ya Kenya**?

.....

(v) (a) Kiri wooni bwaku, kuri maweega ya gutumira **Kiswahili** ta **mugambo ywa kiubici nthiguru ya Kenya**? (Uga **ii** kana **ari**)

(b) Andika itumi bia icookio riaku

.....

.....

(vi) (a) Kiri wooni bwaku, kuri maweega ya gutumira **Gicunku** ta **mugambo ywa kiubici nthiguru ya Kenya**? (Uga **ii** kana **ari**)

(b) Andika itumi bia icookio riaku

.....

.....

(vii) (a) Kiri wooni bwaku, kwombika gutumira **Kiswahili** na **Gicunku** iri **migambo iiri ya kiubici** muno muno ndeene ya cukuru cia mwambiririo (praimari) Kenya?

(Uga **ii** kana **ari**)

(b) Andika itumi bia icookio riaku

.....

.....

(viii) Uumba kuuga atia gukonia uugwe kuumba gutumira migambo iji? (Taara; **kiwango kia iguru, kiwango kia gatigati, kiwango kia nthi**).

(a) Kiswahili

(b) Gicunku

(c) Kimeru

(ix) (a) Ni mugambo juriku ukuthugaania ywateethereria muritwa **kwandikwa ngugi injega** igiita riawe ria nyumene?

(b) Niki?

.....
.....

(x) (a) “Ni ndiikumagiiria gutumira **Gicunku kiubici** nkuruki ya gutumira **Kiswahili**.”

(Uga **ii** kana **ari**)

(b) Andika itumi bia icookio riaku

.....
.....

(xi) (a) “Ni ndiikumagiiria gutumira **Kiswahili kiubici** nkuruki ya gutumira **Gicunku**.”

(Uga **ii** kana **ari**).....

(b) Andika itumi bia icookio riaku

.....
.....

(xii) (a) “Ni ndiikumagiiria gutumira **Kimeru** nkuruki ya **Kiswahili** kana **Gicunku** riria **ndi nja.**”

(Uga **ii** kana **ari**)

(b) Andika itumi bia icookio riaku

.....

(xiii) (a) Kiri **Gicunku** kana **Kiswahili**, ni mugambo juriku ukienda gutumira riria ukwariria mwingi **kiubici**?

(b) Andika itumi bia icookio riaku

.....

.....

(xiv) (a) “Kuri na maweega ya kumenyeera, gukuria na gutaambia **migambo ya gintwire**, ta **Kimeru, Kenya**? (Uga **ii** kana **ari**)

(b) Andika itumi bia icookio riaku

.....

.....

(c) Kiri wooni bwaku, ni itagaaria ririku thirikari ibateerie kujukia kenda yuumba **kumenyeera, gukuria na gutaambia migambo ya gintwire**, ta **Kimeru, Kenya**?

.....

.....

.....

(xv) (a) “Uge bwa o igiita o igiita bwa munene wa kithomo Kenya, Jacob Kaimenyi, ni ati **migambo ya gintwire ni ibwirite itumirwe kuritana aana kuuma nasari mwanka kirasi kia bithatu** kiri mutaratara jwa kithomo Kenya.” Kiri wooni bwaku, iji yoomba kwithirwa iri njira imwe ya kumenyeera na gukuria migambo ya gintwire Kenya? (Uga **ii** kana **ari**)

.....

(b) Andika itumi bia icookio riaku

.....
.....

(xvi) (a) “Kuri na gitumi kia thirikari kumenyeera na gukuria utumiri bwa **Mugambo ywa Mathithio ywa Kenya, Breli** na njira ingi iria ciumba gukinyirika ni **antu baria bari na mawaathe.**” (Uga **ii** kana **ari**)

(b) Andika itumi bia icookio riaku

.....
.....

(c) Kuringana na wooni bwaku, niatia thirikari juumba kumenyeera na gukuria utumiri bwa **Mugambo ywa Mathithio ywa Kenya, Breli** na njira ingi iria ciumba gukinyirika ni **antu baria bari na mawaathe?**

.....
.....

(xvii) (a) Kiri wooni bwaku, ni uriku kiri antu baba ubateerie kuritanwa **Mugambo jwa Mathithio ywa Kenya?** (Ringira icookio riaku musitari).

Itaigua aki Baria baigagua aki Itaigua na baria baigagua

(b) Andika itumi bia icookio riaku

.....
.....

(xviii) (a) Kiri wooni bwaku, kiri antu baba, ni uriku ubateerie kuritanwa **Mugambo ywa kwandika na mutambo ywa Breli Kenya?** (Ringira icookio riaku musitari).

Atumuumu aki Baria boonaga aki Atumuumu na baria boonaga

(b) Andika itumi bia icookio riaku

(xix) (a) Kiri wooni bwaku, kiri **Kiswahili** na **Gicunku**, ni mugambo juriku **jugimarite kimariitwa?**

(b) Niki?

.....
.....
.....

Ni bwega mono niuntu bwa guumpa igiita riaku. Uteethio bwaku buri na gitumi gikinene mono ndeene ja ucunkuuni bubu.

